# ACADEMIE BILIMON




# Kitabu cha Elimu ya Uraia kwa viongozi wa vijana

**Noglo, Koffi Emmanuel na Stein, Margit**

**Desemba 31, 2022**

**Kwa msaada wa kiufundi na kifedha wa Chuo Kikuu cha Vechta na Jimbo la Shirikisho la Niedersachsen**

# Kitabu cha Elimu ya Uraia

# kwa viongozi wa vijana



**Picha ya majaribio ya mafunzo huko Lomé, Togo, 2022**

Kimetayarishwa na „Academie Bilimon"
(www.bilimonacademie.org ), kwa usaidizi wa Maprofesa Taaluma ya Ualimu wa Chuo Kikuu cha Vechta na ufadhili kutoka Jimbo la Niedersachsen..

Lome (Togo) Oktoba, 2022.

# Yaliyomo

**Yaliyomo** .......... **3**
**Dibaji** .......... **7**
**1. Kuanzishwa kwa “Academie Bilimon“** .......... **9**
*1.1. Kuwasilisha “Academie Bilimon“* .......... *9*
Academie Bilimon" ina maono yafuatayo: .......... 9
Kwa kuangalia mitazamo ya kibinafsi na ya kitaaluma kwa mtu binafsi katika nchi yake mwenyewe .......... 10
*1.2. Academie Billimon na ufundishaji wa Paolo Freire.* .......... *10*
**2. . Mawazo makuu ya kazi** .......... **11**
*2.1. Jukumu la jinsia, utofauti na ushirikishwaji katika mafunzo yanayoendelea* *11*
*2.2. Udhibiti wa migogoro na mawasiliano yasiyo ya vurugu kama msingi wa kuendelea na mafunzo* .......... *12*
*2.3. Uwasilishaji wa hali ya kisheria juu ya mafunzo zaidi ya vijana* .......... *12*
**3. . Misingi ya kuunda warsha na mbinu za tathmini** .......... **12**
*3.1. . Maandalizi ya Warsha* .......... *14*
*3.2. Maoni kuhusu mawasiliano kati ya walimu (mabalozi wa elimu) na wanafunzi (washiriki katika tendo la mafunzo endelevu)* .......... *16*
*3.3. Mwanzoni mwa mwongozo huu, ilielezwa kwamba uingiliaji kati wa kujifunza unaoitwa "Approche OLGON" unategemea "ufundishaji wa uhuru" (Paulo Freire). Katika mbinu hii wanafunzi wenyewe huunda maarifa yao.* .......... *16*
*3.4. . Mbinu za tathmini* .......... *17*
*3.5. Mfano wa ripoti ya warsha* .......... *18*
*3.6. Mbinu za kuhamasisha washiriki wakati wa uelimishaji* .......... *18*
*Michezo ya jumla ya motisha na michezo inayohamasisha kufahamiana (Getting to know you games)* .......... *18*
*Michezo ya Kufahamiana.* .......... *20*
**Module 1: Ufuatiliaji wa utambulisho binafsi na wa pamoja kama kikundi** .......... **23**
*4.1. Moduli 1: Kiambata cha utambulisho binafsi na wa pamoja kama kikundi* .......... *24*
*Mbinu za Moduli 1* .......... *24*
Njia ya 1: Nini kinanifanya niwe nilivyo? .......... 24
Kutengeneza Ramani ya Fikra (Mindmaping) .......... 25
*Karatasi ya 2: "Rada ya Utambulisho"* .......... *26*
Njia ya 2: Uundaji wa makundi .......... 27
*Utambulisho unaathiri vipi maisha ya kila siku?* .......... *28*
Njia ya 3 .......... 29
*Karatasi 1: "Mtiririko wa mazungumzo ".* .......... *30*
Njia ya 4: Mkutano wa Utambulisho .......... 32
*Ushawishi* .......... *33*
Njia ya 5: Ushawishi .......... 34
Njia ya 6: Ghiliba .......... 36
Mfano wa genogram: .......... 37
Kazi ya maandishi kuhusu mada ya ghiliba. Karatasi ya 1 .......... 39
Kazi ya maandishi kuhusu mada ya karatasi ya ghiliba Karatasi 2 .......... 40
Kazi ya maandishi kuhusu mada ya karatasi ya ghiliba Maandishi 3 .......... 41
Kazi ya maandishi kuhusu mada ya karatasi ya ghiliba Maandishi ya 4 .......... 42
Taratibu za Ushawishi .......... 43
Njia ya 7: Uzoefu wa ubaguzi .......... 43
Njia ya 8: Ulinzi dhidi ya ushambilizi .......... 45
Njia ya 9: Kukabiliana na ubaguzi .......... 46

Njia ya 10: Wito wa msaada dhidi ya ubaguzi. ....47
Ubaguzi wa rangi na namna ya kuupinga ....50
Moduli 2: Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa kingono....52
*4.1. Ufuatiliaji wa Uwajibikaji wa kingono....53*
Kujenga ukaribu ....55
*Mbinu za Moduli 2....57*
Njia ya 1: Hatua nne za kujenga kujenga ukaribu ....57
*Mtazamo wa mfumo kujenga ukaribu na malezi ....58*
Njia ya 2: Mifano minne ya kujenga ukaribu....59
Njia ya 3: Kutambua hisia....61
Tofauti: ....62
Huruma/Uelewa(Au kujaribu kuvaa viatu vya mwenzako):....63
Njia ya 4: Mazungumzo ya kadi ....63
Njia ya 5: Mwanga wa maoni ....66
Njia ya 6: Nyumba ya mapendo ....67
Njia ya 7: Mwanamke wa ndoto - Mwanaume wa ndoto ....69
Njia ya 8: Ripoti ya Wanawake wajawazito ....70
Njia ya 9: Warsha za ubunifu juu ya ujauzito, watoto na uzazi....73
*Tafakari ya jumla ....74*
" ....74
NJIA YA 10: PICHA ZA BIBI HARUSI NA BWANA HARUSI ....76
Njia ya 11: Kuzuia ukatili wa usawa wa kijinsia. ....77
Njia ya 12: “Wale wote ambao … “....79
Njia ya 13: VVU na UKIMWI ni nini? ....80
Njia ya 14: Vizuia Mimba....82
Uwezekano wa tofauti: ....83
Njia ya 15: Nini kitatokea ikiwa … ....84
*Variation possibilities: ....85*
**Moduli 3: Kufuatilia ili kutambua malengo binafsi ya kitaaluma, kusimamia mpango wa kitaaluma. ....86**
*4.3. Moduli 3: : Kufuatilia ili kutambua malengo binafsi ya kitaaluma kusimamia mpango wa kitaaluma....87*
*Malengo ya maisha yanapatikanaje?....87*
*Mbinu za kutafuta malengo. ....89*
Njia ya 1: Malengo ya maisha, uwanja wa maish....89
Njia ya 2: Dodoso la utafiti juu ya maono ya maisha....90
Njia ya 3: Dodoso la utafiti juu ya hali ya maisha na malengo ya maisha ....92
Njia ya 4: Toleo la baadaye....94
Njia ya 5: Njia ya SMART....95
*Njia ya 6: Nyaraka za malengo ya maisha....97*
Njia ya 7: Kitabu cha Maendeleo....98
Njia ya 8: Matarajio na malengo ya kweli ....99
Njia ya 9: Maana ya malengo....101
Njia ya 10: Majaribio ya mawazo....103
**Moduli 4: Kuambatana na Kujitolea kwa Jamii ....105**
*4.4. Module 4: Kuambatana na Kujitolea kwa Jamii ....106*
*Mbinu za Moduli ya 4....107*
Njia ya 1: Tunahitaji kiasi gani?....107
Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ....113
Njia ya 2: Picha nyingine ya kioo....114
Njia ya 3: „ Ninachotaka na kile ninachofanya....116

Njia ya 4: I—(Mimi) Maelezo ....119
Vifaa: ....121
Njia ya 5: : Kikaragosi....122
Vifaa: ....125
Njia ya 6: Maisha duniani ....127
Njia ya 7: Mtandao wa buibui ....130
Njia ya 8: : Kipindi cha mazungumzo (talkshow) ....131
Njia ya 9: Muhtasari wa majukumu ....133
Njia ya 10: Mjadala wa kuunga na kupinga hoja ....134
*Maswali/hoja zinaweza kuwa:....136*
*Ujuzi wa msingi wa usimamizi wa migogoro ....137*
*Mgogoro unaibuka vipi?....138*
*Usimamizi wa migogoro ni nini? ....138*
*Migogoro inawezaje kutatuliwa na kuzuiwa? ....138*
Ukatili/Vurugu ....139
*Aina za vurugu....139*
Njia ya 11: Kuingilia kati na mbinu dhidi ya ukatili ....141
(https://www.researchgate.net/profile/Albert-....141
*Mawasiliano ....143*
*Nini maana ya mawasiliano yasiyo ya vurugu? ....144*
*Mtu anachukuliaje mawasiliano yasiyo ya vurugu? ....144*
*Marshall B. Rosenberg - Mawasiliano yasiyo ya vurugu....145*
Njia ya 12: Mfano wa hatua nne....145
*Hatua ya 1: Uchunguzi ....146*
*Hatua ya 2: Hisia ....146*
*Hatua ya 3: Mahitaji ....146*
*Hatua ya 4: Hatua / Ombi / Matakwa ....147*
*Marshall B. Rosenberg anatofautisha kati ya ngazi tatu za mawasiliano:....149*
Selbst-Einfühlung: ....149
*Kusikiliza kwa uelewa ....149*
*Usimamizi wa migogoro unawezaje kutumika kuleta mawasiliano yasiyo ya vurugu?....150*
*Mfano wa barafu ....150*
*Dhana ya Harvard....152*
Njia ya 13: Udhibiti wa Migogoro:....153
Mfano wa Utatuzi wa Migogoro ....153
Hatua ya 1: Fafanua maoni ....153
*Hatua ya 2: Funua kusudi lililobeba maoni ....153*
*Hatua ya 3: Tambua wasiwasi wao mkuu.....154*
*Hatua ya 4: Fafanua umuhimu wa mambo yanayoleta wasiwasi.....154*
*Hatua ya 5: Andaa ufumbuzi wa msingi wa suala.....154*
*Hatua ya 6: Kuchagua suluhisho bora. ....154*
*Maneno ya kufunga ....155*
*Vifaa vya kazi kutoka Moduli ya 1 ....156*
Muhtasari: Hisia za msingi ....159
Picha kwa hisia....166
Vifaa vya kazi kutoka Moduli ya 4: Kuhusu usimamizi wa migogoro ....174
*Orodha ya hisia....174*
*Orodha ya mahitaji....175*
*Tambua mahitaji ....175*
*Historia ya kuelewa hisia ....176*

*Kuandaa maombi*......178
*Kuelewa mgogoro*......180
Abbildung nach Holler, 2016, p.196 ......180
**Kuvuka ziwa......182**
**Bibliography (a selection)......183**

## Dibaji

Kitabu hiki cha mwongozo wa semina ni mahususi kwa mabalozi wa elimu wa "Academie Bilimon", pamoja na mashirika yaliyojikita katika kutoa elimu ya siasa kwa vijana. Makala haya ni matokeo ya ushirikiano kati ya maprofesa wa Taaluma ya Ualimu (Chuo kikuu cha Vetcha - Uni Vechta) na "Academie Bilimon", na yanachukuliwa kama mafunzo ya kazi za siasa pamoja na kwa vijana. Kabrasha hili lenye moduli nne limeundwa kwa ajili ya kutumiwa na wananchi wote ili kuepusha ile hali ya utengano (sio tu kidini) ili kuunda jamii/raia liwe jukumu la wote. Kitabu hiki kwa "mijadala yakinifu" (Hartkemeyer, 2016) inaweza kuwa fursa na kuasiliwa kukidhi muktadha na tamaduni za jamii tofauti tofauti ili maudhui yaliyobebwa na kitabu yalete manufaa hasa mabadiliko ya kazi ya siasa kwa maana ya Montesquieus.

Matumizi zaidi yanaweza kufuata ili kuendeleza roho ya kazi ya elimu ya Paulo Freire (ufundishaji wa uhuru), ambayo ni msingi wa kazi ya elimu ya "Academie Bilimon". Uundaji wa kitabu hiki umehusisha Wataalam tofauti, na ni vigumu kuwataja wote hapa. Hata hivyo, ni muhimu kuwataja wahusika wakuu, maana bila mchango wao adhimu kitabu hiki kingeishia kwenye makabrasha ya ofisi;

Miongoni mwao ni Profesa Margit Stein, Mwanachama wa Bundestag Susanne Menge, mabalozi wa elimu wa "Academie Bilimon" kama vile Djifa Kokou Adjim, Mawuli Assimadi, Hervé Awui Talla, Dominique Kwassi Edoh, Jean-Mari Lawson, Immaculée Sambiani, Emmanuel Magar Yayoune, pamoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Vechta kama vile Merit Beckmann, Meawiya Othman, Yasima Köhne, Sikran Agirman, Vanessa Strieker, Aileen Gewohn, Katharina Wilke, Stefan Rösecke, Franziska Baven diek, Malte Kotmann, Deliah Toma, Adrian Niesch, Martha Kroop, Michelle Sauer, Jana Golak, Chantal Wellmeyer, Amy Ellis, Nico Richter, Thi Thuy Nhung Bui, Jana Naibauer, Sönke Peinz, Jonathan Kolks, Birte Grote, Sophia Wienhold, Tatjana Wiechers, Tobias Arfmann, Anneke Harland, Julia vonje Sparder Ohe na Franziska Baumeister.

Shukrani za pekee pia kwa jimbo la Lower Saxony, ambalo lilisaidia mradi huu kifedha.

Vuguvugu la "Fridays-for-future" (ambalo sasa linaenea katika mabara) ni dalili kwamba vijana wemeamka na wanataka kuchukua hatua fulani za kuunda

ulimwengu kwa mikono yao wenyewe, au angalau wawe na mwelekeo mzuri wa maisha yao wenyewe.

"Pedagogy of Autonomy" ya Paulo Freire, the basis "Approche OLGON" (inatoa ufafanuzi zaidi kuhusu mfumo huu wa kutoa elimu), ambayo inaelekeza kazi ya elimu-kiraia ya "Academie Bilimon", ambayo inafundisha vijana kwa njia ya mipira theluji “snowball system” ili waweze kuchangia kikamilifu na bila vurugu kuunda hatma yao ya baadaye.

Ni vema watendaji wanawake zaidi na zaidi waunge mkono mwelekeo huu wa kidemokrasia unaoanzia katika ngazi ya jamii ili ile hali ya mtu kuona mchango wake umethaminiwa na mfumo mzima uendelee kukua katika kizazi cha vijana.

Dk Koffi Emmanuel Noglo

Bamako, Septemba 24, 2022

## 1. Kuanzishwa kwa "Academie Bilimon"

### 1.1. Kuwasilisha "Academie Bilimon"

"Academie Bilimon" ilianzishwa na wafadhiliwa kutoka Togo waliopata ufadhili kutoka Protestant Development Service EED (Bread for the World) ambao walisoma na kufanya tasnifu yao nchini Ujerumani na Ufaransa na walitaka kuchangia kazi ya elimu ya siasa nchini Togo, kama mchango wa maendeleo ya nchi yao. Waanzilishi wote (Dkt. Koffi Emmanuel Noglo na Kossi Gbati Agbo) sasa wanafanya kazi Bamako (Mali) na Abidjan (Côte d'Ivoire). Pamoja na ofisi iliyoko Lomé (Togo), Academie Bilimon ina eneo Munich (Ujerumani) yenye tovuti (bilimon.de au bilimonacademie.org).

Jina la "Academie Bilimon" linatokana na neno "Bilimon", lililochukuliwa kutoka lugha ya Bassar inayozungumzwa kaskazini mwa Togo. "Bilimon" inamaanisha "Ni bora watu wawili wakitenda". Jina "Bilimon" ni kielelezo cha dira ya mshikamano na kuheshimiana, maadili ambayo yanawakilishwa katika "Académie Bilimon" ambayo inaambatana na vijana katika kujifunza mshikamano wao wenyewe na kuweza kuutekeleza kwa vitendo miongoni mwao. Vijana ambao wamekulia chini ya muundo wa kijamii, kitamaduni na kiuchumi wa vurugu mara nyingi hupoteza hisia zao za uwajibikaji na imani na mfumo.. Kwa sababu hii, "Bilimon" sio tu jina, bali ishara ya kuwakusanya upya vijana katika dhana ya kila mtu kuwajibika na mshikamano, kwa msingi ambao maendeleo endelevu ya kijamii yanaweza kupatikana.

**Academie Bilimon" ina maono yafuatayo:**

- ✓ Kuwa nafasi ya kukutana kwa na kutoka kwa vijana;
- ✓ Kuimarisha hali ya kujiamini na imani katika kundi la vijana;
- ✓ Uwazi au usikivu kwa vijana wote, bila kujali hali ya mtu kijamii, dini, kabila na elimu.;
- ✓ Kanuni ya upamoja wa hiari na kukuza ushiriki wa mtu binafsi kijamii na wenzao au mabalozi wa elimu wa "Academie Bilimon".

## Kwa kuangalia mitazamo ya kibinafsi na ya kitaaluma kwa mtu binafsi katika nchi yake mwenyewe

Kwa mujibu wa wasifu na taswira ya nchi, "Academie Bilimon" inataka kuwa mahali pa kukutania kwa ajili ya kazi ya elimu ya siasa kwa vijana au kuunda nafasi kama hiyo, ambapo vijana wanasindikizwa kwa namna ambayo wataweza kujifunza mambo mengi kila mmoja “akipanuka kififikra” na kuwa na "mzunguko wa fikra" ndani ya bara lao. Hii itasaidia kuondoa “ufinyu wa fikra” kwa mfano kupunguza vijana wengi kuhamia nje kunaweza kuepukwa. Kwa hiyo, vijana wanaweza kuepuka mateso ya kihisia wanapozuiliwa mipakani wakijaribu kwenda ng’ambo na badala yake wajione kama raia wa dunia ambao wako tayari kuingilia changmoto za jamii zao na kuchangia maendeleo endelevu, hata kama wanakaa ughaibuni kwa muda mfano Munich, Paris, Vechta, Marburg, Geneva. Nancy, Lomé, Niamey au mahali pengine.

Ili kuhakikisha maono haya na wasifu huu vinaweza vinapatikana, "Academie Bilimon" imejiwekea jukumu la kuwaelimisha au kuwawezesha vijana kisiasa na kijamii katika aina ya utafiti wa vitendo ili wawe washiriki wa maendeleo yao wenyewe na maendeleo endelevu ya jamii yao. Shughuli zote, miradi na programu za "Academie Bilimon" zinaheshimu mtazamo huu wa kimsingi wa uwajibikaji na uwezeshaji.

Kwa mantiki hiyo Mtazamo wa kiraia wa "Academie Bilimon" unaweza kusomwa kupitia lenzi ya mbinu ya ushirikiano wa maendeleo "msaada wa kujisaidia" (help for self help) na kufupishwa katika sentensi ifuatayo: "Jizoeze kutenda ili ujisaidie na usaidie wengine, ndipo utatoa mchango wako  kwa jamii au mfumo unaojenga kujiamini na kujitambua". Inapaswa kutajwa hapa kwamba matokeo  kazi ya utafiti iliyotolewa na mwandishi wa makala haya, Koffi Emmanuel Noglo, mwaka wa 2012 katika kitabu ‚Die Legitimität des Staates im multiethnischen Kontext – Der Fall. (The Legitimacy of the State in a Multiethnic Context - The Case of Togo), ndio msingi wa kitabu hiki na ni msingi wa kisayansi wa kazi za Academie Bilimon.

### 1.2. Academie Billimon na ufundishaji wa Paolo Freire

Paulo Freire "Pedagogy of Autonomy" (2013) unachukuliwa kuwa msingi wa kazi zaidi ya elimu ya "Academie Bilimon". Kimsingi, mbinu hii ni kuelewa kwamba wanafunzi wanajisikia kusindikizwa kuanzia kwanye udadisi wao wa kutojua hadi udadisi wa kielimu, ambapo maarifa hujengwa na wanafunzi wenyewe. Mtazamo huu husaidia "Academie Bilimon" kuvunja matabaka (hierarchies) na kuchangia kuongezeka kwa

ukomavu. Hii inaiwezesha"Academie Bilimon" kujiweka kitaasisi kati ya mfumo wa shule au elimu ya chuo kikuu na kitaaluma au maisha ya kila siku ya vijana.

"Ufundishaji huu wa uhuru" uliasiliwa na tamaduni za ndani ya nchi husika sambamba na maandishi ya Freire yaliyoitwa "Approche OLGON": Msingi wa aina hii uliofafanuliwa zaidi wa "ufundishaji wa uhuru" ni kuambatana na wanafunzi ili kuwawezesha kuhama kutoka kutokujua hadi udadisi wa kielimu. . Kuna mwelekeo dhabiti kuelekea maisha ya kila siku ya wanafunzi, kwa mfano kwa kusogeza mafunzo chini ya kivuli cha mti au kwenye sehemu ya mikutano au klabu ya vijana ya eneo hilo. Kusudi la ausiliaji huu wa kikanda na wa hali ni kujenga ukweli wa kijamii ili utekelezaji wake usikinzane na muktadha wa muhusika. Kwa njia hii, washiriki wenyewe wanaweza kuwa washiriki wakuu wa maendeleo yao wenyewe na maendeleo ya jamii yao, kupata heshima kwa maarifa waliyoyapata, na kuanzisha mazungumzo kati ya miundo ya kijamii iliyozalishwa tena na matarajio yao ya maendeleo.

## 2. . Mawazo makuu ya kazi

### 2.1. Jukumu la jinsia, utofauti na ushirikishwaji katika mafunzo yanayoendelea

Katika ulimwengu ambapo ubaguzi (sio wa kidini pekee) unakubalika na hasa nchi kama Togo, ambapo masuala ya kikabila yana nguvu kisiasa na kiutawala, vipengele vinavyovuka mipaka kama vile jinsia, utofauti na ushirikishwaji vinapewa umuhimu.

Katika moduli zote nne za warsha, hasa katika suala la utambulisho (iwe unahusiana na mtu binafsi au kwa jamii), uangalifu unachukuliwa ili kuhakikisha kwamba walengwa wanafahamishwa kwamba katika historia ugomvi kwa sababu tu ya tofauti mara nyingi imesababisha uharibifu wa pande zote. Kwa kuwa sababu zinazofanana mara nyingi husababisha athari sawa, wasitarajie matokeo tofauti pindi wanashambuliana (iwe ni kwa kujua au pasipo kujua). Ni muhimu ifahamike mwanzo kabisa kwamba "Academie Bilimon" haiwashawishi walengwa kutenda kwa njia fulani. Kimsingi wanafahamishwa kuwa kila tendo lina athari zake. Kwa hiyo ni vyema kwao kufikiria kwa makini kabla ya kutenda na kukubali kuwajibika kwa matokeo ya matendo yao..

### 2.2. Udhibiti wa migogoro na mawasiliano yasiyo ya vurugu kama msingi wa kuendelea na mafunzo

Msemo wa Ewe "Vibuyu viwili kwenye uso mmoja wa maji haviwezi kuepuka kugusana" Migogoro kati ya watu haiepukiki. Katika kazi ya elimu ya "Academie Bilimon", uangalifu unachukuliwa ili kuhakikisha kwamba walengwa wanajifunza kutatua migogoro hii bila kutumia vurugu. "Academie Bilimo" katika warsha inafundisha mbinu ya walengwa daima kujiangalia wao ni kwa jinsi gani wamechangia kusababisha mgogoro, badala ya mara nyingi kutafuta makosa kwa wengine. Vikundi vinavyolengwa pia hujifunza kuwasiliana kwa njia isiyo ya vurugu (kwa uchaguzi wa maneno sahihi) ili petroli isimwagike kwenye moto wa migogoro..

### 2.3. Uwasilishaji wa hali ya kisheria juu ya mafunzo zaidi ya vijana

Kwa ujumla watoto na vijana wanalindwa nchini Togo na Sheria Na. 2007-017 ya Julai 6, 2007 (ambayo ilichukua nafasi ya sheria zilizokuwa zikitumika hadi wakati huo). Wakati huo huo, sheria inatoa haki ya watoto kukuzwa. Vifungu kama vile haki ya jina (Na. 10), haki ya uraia - inatosha kwa mtoto kuzaliwa Togo (Na. 18), haki ya nyumba (No. 25, 26 na 27), haki ya urithi kwa watoto wote kwa usawa, bila ubaguzi wa jinsia (Na. 114), haki ya elimu (Na. 149), ya afya (Na. 240), ya hifadhi ya jamii (Na. 244), lishe bora (No. 245), ya mafunzo ya ufundi (No. 256), ya elimu ya kitamaduni, na burudani (No. 259), nk. Sheria hii ni msingi wa kazi ya elimu ya "Academie Bilimon".
"Academie Bilimon" daima inahakikishwa kuwa mabalozi wake wa elimu wanatenda ndani ya mfumo wa mwelekeo huu wa kisheria, ambao haubagui mtu yeyote.
Sasa baada ya kuelezea Academie Bilimon na kazi yake ya elimu ya uraia, inafaa kutazama kiini cha ujumbe wake miongoni mwa vijana..

## 3. . Misingi ya kuunda warsha na mbinu za tathmini

Mpangilio wa warsha za "Academie Bilimon" umejengwa katika dhana ifuatayo: Raia anayejiamini, anawajibu wa kingono, anajua jinsi ya kutekeleza mipango yake ya kitaaluma na kuelewa maana ya kanuni ya kundi kijamii, na ana uwezekano mkubwa wa kuwa na mchango katika maendeleo endelevu ya jamii yake.
Dhana hii inatokana na uchunguzi wa washiriki nchini Togo kama sehemu ya tasnifu ya uzamili (2007) na ziara tatu za utafiti (majira ya baridi 2009/2010, majira ya baridi 2010/2011, na kiangazi 2011) kama sehemu ya tasnifu ya udaktari ya Koffi Emmanuel Noglo. Matokeo ya utafiti huu yalijumuishwa kwa kiasi katika kitabu cha 'Die Legitimität

des Staates im multiethnischen Kontext – der Fall Togo (Noglo, 2012). Yafuatayo ni matokeo yaliyoibuka:

**Swala la utambulisho nchini Togo** mara nyingi hujadiliwa kulingana na masuala ya kikabila na historia ya kusikitisha ya utumwa na ukoloni. Hakuna jaribio lolote la kujadili swali hili ndani ya mfumo wa mipango ya kiraia ambayo inaweza kusaidia nchi kufuata mwelekeo wake wa maendeleo ya kitafa ulio dhahiri au utashi wa kitaifa.

**Tabia ya kingono ya mtu binafsi** haitokani na uelewa wa uhusiano kati ya sababu na matokeo (a cause and effect). Mara nying vijana hawana ufahamu wa kutosha kuhusu athari au matokeo ya tabia zao za kingono (kwa mfano, mimba za mapema, magonjwa ya zinaa, nk) na familia au jamii pasipo kuelewa kuwa vijana hawakupewa kujenga ukaribu katika makuzi yao ya kingono, wanakua wakali sana kwa vijana wiliopata athari hizo..

**Swali la malengo ya ajira** halijadiliwi mapema na wanafunzi au vijana. Swali hili linakuja tu wakati wanakaribia kuchukua diploma ya vidato vya juu au hata baada ya hapo. Athari za wakati huu uliopotea bure ni mpaka kwenye aina ya ajira mtu anafanya na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**Sheria za kijamii hazitiliwi shaka** Sheria za kijamii hazitiliwi shaka

- **Moduli ya 1: Uambatanisho wa mtu kujitambua binafsi na utambulisho wa pamoja (au utambulisho binafsi na mambo yanayotuweka pamoja: na nini kinachounganisha vyote viwili? Mivutano iliyopo/uzoefu/ hutekelezwa vipi?).**
- **Moduli ya 2:** Kufundisha wajibu wa kingono. Moduli hii ni muhimu kwa sababu "Academie Bilimon" inafanya kazi katika jamii ambapo ongezeko la idadi ya watu halifuati uzazi wa mpango, kuna mimba za mapema sana na ndoa za utotoni, pamoja na ukosefu wa haki sawa kwa wanawake, vinaathiri vibaya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.
- **Moduli ya 3: Mwongozo wa kutambua malengo ya mtu binafsi kitaaluma na ya kibinafsi na kusimamia mpango binafsi wa kitaaluma.** Moduli hii inatoa mafunzo ya ufundi ambao husaidia vijana kutengeneza na kutumia zana za usimamizi wa mradi katika mipango yao ya kitaaluma.
- **Moduli ya 4: Kuambatana katika ushirika kijamii.** Katika moduli hii ya mwisho, vijana wanafunzwa kuelewa maana na umuhimu wa kanuni na sheria katika kundi la kijamii au nchi na kuweza kuzifuata. Moduli hii inalenga kurejesha imani ya vijana katika mfumo wa kisiasa na kijamii, pamoja na kutoa

ulinzi kwa watu wote wanaoishi katika mfumo wa kijamii uwe wazi zaidi, ili waweze kuheshimu mambo yanayowaweka pamoja. Moduli hii pia inajumuisha kazi ya kupinga ubaguzi, mafunzo ya tamaduni tofauti, mafunzo ya uvumilivu na elimu kwa maendeleo endelevu (ESD).

- **Ili kuhakikisha kuwa matokeo yaliyofikiwa yanakaa kwa muda mrefu na endelevu ndani ya vikundi lengwa kutakua na "mafunzo ya wakufunzi".** Hapa, vijana wakubwa na wadogo hufunzwa kuwa mabalozi wa elimu ambao hupeleka uzoefu na utaalamu wao, maarifa na ujuzi kwa vijana wengine kwa njia ya "elimu rika". Mkazo "Academie Bilimon" pia uko kwenye "mafunzo ya kudumu", yaani, usaidizi wa kudumu kwa walengwa, ikiwa wangependa kutumia usaidizi huu.

### 3.1. . Maandalizi ya Warsha

Kwa kawaida warsha huchukua wiki moja. Timu ya mabalozi wa elimu mara nyingi hukutana kabra ya warsha ili kuratibu hatua za uelimishaji. Maswali ya msingi hufafanuliwa, ikiwa ni pamoja na:

- Ni kundi gani la walengwa linatarajiwa (umri, kiwango cha elimu),
- Uratibu wa hatua za uelimishaji utafanyika lini, wapi na kwa lugha gani,
- Je, utaratibu wa utoaji wa chakula utakuwaje (kutoa wenyewe au kulipia kwa watoa huduma)?
- Je, ni nani atafadhili uratibu wa hatua za uelimishaji (kikundi chenyewe au mfadhili),
- Je, washiriki watafikaje kwenye eneo la warsha?
- Je, majukumu ya utekelezaji wa hatua za uelimishaji yanagawanywaje n.k?

Baada ya yote haya kufafanuliwa, utayarishaji wa yaliyo ndani ya somo huanza. Kama kanuni ilivyo, kwa kila moduli lazima kuna wataalam wa elimu kati ya mabalozi wa elimu, ambao hushiriki moduli 4 kati yao. Timu ya warsha kwa kawaida huwa na mabalozi 5 wa elimu wanaosaidiana wakati wa utekelezaji wa hatua ya elimu.

Jedwali lifuatalo linaonesha mfano wa mchakato wa warsha:

| Siku/Tarehe | Muda | Yaliyomo | utaratibu | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| Siku 1 | | Kupasha Joto (WUP): Sehemu ya washiriki kufahamina katika mduara. | Michezo ya kuhamasisha ya kitabu. Viongozi wa vijana | Mabalozi wa Elimu wa Chuo cha Bilimon |
| Siku 1 | | Uwasilishaji wa "Academie Blimon" | Uwasilishaji wa "Academie Blimon" wasilisho la Power Point la "Academie Bilimon" au wasilisho la kimchezo lenye nadharia ya kazi za "Academie Bilimon" kama sehemu ya kuanzia. | Mabalozi wa Elimu wa Chuo cha Bilimon |
| | | | | |
| Siku 2 | | Moduli ya 1: Utambulisho na tathmini mwishoni mwa siku. | Mbinu zilizowasilishwa katika mwongozo huu viongozi wa vijana, pamoja na michezo ya motisha. | Mabalozi wa Elimu wa Chuo cha Bilimon |
| | | | | |
| Siku 3 | | Moduli ya 2: Uwajibikaji wa kingono na tathmini mwisho wa siku. | Mbinu zilizowasilishwa katika Kitabu hiki cha Mwongozo wa Kiongozi wa Vijana, pamoja na michezo ya uhamasishaji | Mabalozi wa Elimu wa Chuo cha Bilimon |
| | | | | |
| Siku 4 | | Moduli ya 3: Kuambatana katika kutambua na kusimamia mradi wa kitaaluma, na tathmini mwisho wa siku. | Mbinu zilizowasilishwa katika Kitabu hiki cha Mwongozo wa Kiongozi wa Vijana, pamoja na michezo ya uhamasishaji. | Mabalozi wa Elimu wa Chuo cha Bilimon |
| | | | | |
| Siku 5 | | Moduli ya 4: Kuweka msisitizo wa kanuni katika kikundi kijamii na tathmini ya jumla ya warsha. | Mbinu zilizowasilishwa katika Kitabu hiki cha Mwongozo wa Kiongozi wa Vijana, pamoja na michezo ya uhamasishaji. | Mabalozi wa Elimu wa Academie Bilimon |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Day 5 | | Chuo cha Bilimon. Mwaliko wa washiriki kwa ajili ya usambazaji wa maadili kwa ajili ya kuishi pamoja: kupanga shughuli za kuongeza uelewa kwa ushiriki wa vijana katika shughuli za kiraia | Mbinu zilizowasilishwa katika Kitabu hiki cha Mwongozo wa Kiongozi wa Vijana, pamoja na michezo ya uhamasishaji. | Mabalozi wa Elimu wa Academie Bilimon |

NB: Ni uamuzi wa kila timu kuamua kukamilisha au kuliasili jedwali kutokana na hali. Ni muhimu kutenga muda kila siku kwa ajili ya kifungua kinywa, chakula cha mchana, chakula cha jioni na vipindi vya mapumziko (asubuhi na alasiri). Timu ya warsha hukutana kila mwisho wa siku kwa ajili ya tathmini ya siku ya warsha na mapendekezo ya kuboresha siku inayofuata. Tathimini ya uratibu wa siku katika timu ya warsha, hali na mazingira katika kikundi cha washiriki, maudhui ya moduli husika, nk.

**3.2. Maoni kuhusu mawasiliano kati ya walimu (mabalozi wa elimu) na wanafunzi (washiriki katika tendo la mafunzo endelevu)**

**3.3. Mwanzoni mwa mwongozo huu, ilielezwa kwamba uingiliaji kati wa kujifunza unaoitwa "Approche OLGON" unategemea "ufundishaji wa uhuru" (Paulo Freire). Katika mbinu hii wanafunzi wenyewe huunda maarifa yao.**

Maoni kuhusu mawasiliano kati ya walimu (mabalozi wa elimu) na wanafunzi (washiriki katika tendo la mafunzo endelevu)

Mwanzoni mwa mwongozo huu, ilielezwa kwamba uingiliaji kati wa kujifunza unaoitwa "Approche OLGON" unategemea "ufundishaji wa uhuru" (Paulo Freire). Katika mbinu hii wanafunzi wenyewe huunda maarifa yao.

Kwa hiyo, walimu wanatarajiwa kuandaa mazingira stiri kwa ajili ya mchakato wa kujifunza. Ni muhimu sana kuepuka kulazimishia wanafunzi kitu kilichoandaliwa, bali kuambatana kwa namna ambayo watapata maarifa (mapya) kutokana na juhudi zao

wenyewe katika mchakato wa kujifunza. Kitu ambacho wanaweza kutumia katika maisha yao ya kila siku.

Kwa mfano, inatarajiwa kwamba katika moduli zote wanafunzi wenyewe wawe na uelewa kuhusu:

- **Moduli ya 1:** Utambulisho wangu unapaswa kupatana na utambulisho wa wengine ili tuishi pamoja kwa amani;
- **Moduli ya 2**: Maisha yangu ya ngono yanaweza kuathiri mipango yangu ya kitaaluma chanya au hasi, kulingana na hali ninayopitia;
- **Moduli ya 3:** Maisha bila mipango ya kitaaluma, utekelezaji na tathmini yanaweza kuwa na matokeo mabaya katika suala zima la kuridhika kwa mtu maishani. Katika hatua hii, mbinu za usimamizi wa mradi zinaoneshwa kwa wanafunzi ambazo wanaweza kuzitumia katika maisha yao wenyewe;
- **Moduli ya 4:** Kuishi pamoja bila kuelewa kwamba kikundi au jamii lazima ikubaliane na kufuata sheria zinazowaweka pamoja kunaweza kusababisha machafuko na kutokuwa na furaha kwa wote.

Jukumu kuu la walimu ni kuwaongoza washiriki kwenye njia ya uhakika huu, pasipo kulazimishia uhakika huo. Utamaduni wa "kidemokrasia" wa mawasiliano katika kujifunza ndio msingi wa kazi ya elimu ya kisiasa ya "Academie Bilimon".

Huenda baadhi ya makundi lengwa hayafikii hakika ya ukweli huu mwishoni mwa mchakato mafunzo. Hata ikiwa inasikitisha walimu, uelewa huu lazima ukubalike; kwa kutambua kwamba kundi hili bado linahitaji muda wa kuelewa maana ya wajibu wao wenyewe kwa maendeleo yao na maendeleo ya wote. Inahitajika jitihada zaidi katika kuambatana na kikundi kama hicho.

Kwa sababu, maendeleo ya mtu au maendeleo ya jamii hayaji kwa kulazimishiwa. Yanakuja kwa jitihada za mtu/watu wenyewe..

### 3.4. . Mbinu za tathmini

Mbinu mbalimbali zinatumika ili kujua ni nini kimekwama katika makundi lengwa: Hojaji (kabla na baada ya jaribio la yaliyomo kwenye warsha), Vikundi kujadiliana kuhusu yaliyomo kwenye warsha na uwasilishaji wa matokeo kwa jumla.

Mwishoni mwa kila warsha, timu ya elimu huandika ripoti, ambayo inakusudiwa, kati ya mambo mengine, kupitisha mapendekezo ya maboresho ya maudhui na mpangilio

wa "Academie Bilimon". Jedwali hapa chini linaonesha sampuli ya ripoti ya warsha, ambayo haipaswi kuwa ndefu sana: takriban kurasa 5..

### 3.5. Mfano wa ripoti ya warsha

Ili vijana wawe na modeli ya kuripoti kwa vitendo, "Academie Bilimon" imetengeneza jedwali lifuatalo.

| | | |
|---|---|---|
| **Académie Bilimon pour la Recherche et le Développement Participatif (ABREDEP** | Aina ya shughuli (Tendo) | |
| | Kundi lengwa | |
| | Idadi ya washiriki (kugawanywa katika wanawake na wanaume) | |
| | Idadi ya kurasa za ripoti | |
| | Mwandishi wa ripoti hiyo | |
| | Tarehe ya kuripoti | |
| | Mahali pa tendo | |

| **Maudhui ya ripoti** |
|---|
| Muhtasari wa maudhui ya tendo hilo: |
| Mipango ya shughuli za ufuatiliaji: |
| Baadhi ya mambo muhimu wakati wa warsha hiyo: |
| Mapendekezo kwa "Academie Bilimon": |
| Kiambatanisho (picha za warsha): |

### 3.6. Mbinu za kuhamasisha washiriki wakati wa uelimishaji

Michezo ya motisha ni muhimu sana wakati wa kutoa elimu kwa vijana kwa sababu huwahamasisha kukaa makini wakati wote wa warsha. Njia hii ya kujifunza kupitia michezo inapokelewa vizuri na vijana. Kila siku, vikundi lengwa huandaa michezo mpya ya motisha, ambayo hurutubisha sanduku la michezo ya hamasa la "Academie Bilimon".

Katika kurasa zifuatazo, mifano ya baadhi ya michezo ya hamasa, pamoja na mbinu zake, huwasilishwa. Zimekusanywa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Vechta na kugawanywa (kati ya zingine) kwa moduli 4 husika.

**Michezo ya jumla ya motisha na michezo inayohamasisha kufahamiana (Getting to know you games)**

Michezo ya Getting to know you hutumiwa mwanzoni kabisa mwa mafunzo kabla wanakikundi hawajafahamiana vizuri. Hakuna mipaka ya mawazo linapokuja suala la kufahamiana. Jambo la muhimu zaidi ni lengo ninalonuia kulifanikisha pamoja na

kikundi. Washiriki wanapaswa kufahamu kundi lao katika awamu tofauti za kuwa pamoja, kupunguza vizuizi na kujenga nguvu ya kikundi. Haijalishi ni aina gani ya kikundi. Watoto, vijana na watu wazima wote wanapaswa kufahamiana tena wakati muundo wa kikundi ni mpya.

Ni muhimu kukumbuka kwamba kila kundi ni tofauti, na mchakato unaweza kuchukua muda tofauti hadi kikundi kitakapopatana vizuri.

Mchezo wa kufahamiana (Getting to know each other) inafaa sana kwa mikutano ya kwanza ya vikundi vipya, kwani mara nyingi inaweza kuchezwa bila kuongeza nyenzo. Hii inamaanisha kwamba zinaweza kutumika mahali popote. Zinaweza kuchezwa nje na ndani na zinaweza kutumika kwa karibu na kikundi cha kila rika.

Michezo ya kujifunza inaweza kuwa imejaa vitendo, na inaweza pia kujaa habari sana. Michezo ya kujifunza ni rahisi sana na inaweza kuhitaji vifaa vichache sana au isihitaji kabisa. Kwa hivyo inaweza kutumika kwa urahisi ukiwa umesafiri. Kwa ujumla, zinafaa kwa madhumuni tofauti tofauti. Michezo kwa watoto pia inaweza kuchezwa na watu wazima. Michezo ya kufahamiana inafurahisha nje au ndani na wala haijalishi idadi ya washiriki, liwe kundi kubwa au dogo wote wote wanaweza kupata mengi ndani ya mchezo. Michezo ya chemsha bongo inafaa hasa kwa mafunzo ya kumbukumbu. Kiwango cha ugumu kinaweza kutofautiana na kuasiliwa na kundi la umri. Lakini sio tu kumbukumbu ambayo ina changamoto, lakini pia ujuzi.

**Michezo ya Kufahamiana**

**Mzunguko wa uwasilishaji – anza kwa hamasa (jump start)**

Tofauti katika makundi ya umri

Kushuka kwa kiwango cha ugumu

Muda unaohitajika: angalau dakika15

maandalizi/vifaa: karatasi, kalamu, chombo

**Kiwango cha ugumu: rahisi**

**Malengo**: Kuimarisha uwezo wa kumbukumbu na uhusiano kati ya picha na neno. Kukuza ujuzi wa kuzungumza na kusikiliza kwa makini. Kadhalika, washiriki wanapaswa kuacha kuona soni na kuzungumza kwa uhuru katika kikundi..

**Makundi ya umri:** Haijalishi umri.

**Kiwango cha utata:** Kiwango cha utata kipo chini. Ugumu kidogo unaweza kuwepo maana washiriki wanapaswa kufunguka kwa kikundi na kujielezea wao wenyewe mbele ya kikundi. Kiwango cha ugumu kinaweza kupunguzwa kwa kuwapa washiriki makundi ya maswali ambayo wanaweza kuchagua. Makundi ya 1-3.

**Muda unaohitajika:** Kulingana na ukubwa wa kikundi na kiwango cha masimulizi, kuanzia takriban dakika 15.

**Ukubwa wa kikundi**: Inafaa kwa vikundi vya watu 8 au zaidi

**Awamu za elimu**: Njia hii inaweza kufanya kazi kama mchezo wa utangulizi ili kuunganisha washiriki na kukifahamu kikundi kwa ujumla.

**Maandalizi / vifaa**: Ili kuandaa mchezo, unahitaji makundi au maswali tofauti mapema ambayo yanaweza kutumika kama mwongozo. Maswali haya yanaweza kuandikwa kwenye vipande vidogo vidogo vya karatasi ambavyo vimekunjwa na kuwekwa kwenye sanduku. Kwa hiyo, karatasi, kalamu na sanduku vinapaswa kutolewa.

**Utaratibu / Maelekezo**: Maelekezo: Je ninawezaje kuanza uwasilishaji? Kwa kawaida, watoto hupata shida kujielezea wao wenyewe. Mara nyingi, kila mmoja wao huishia kusema karibu sawa na wasemaji waliomtangulia. Bila shaka, mzunguko wa mawasilisho ni njia bora ya kujuana. Hata hivyo, washiriki wengi mara nyingi hawajui nini wanaweza kusema juu yao wenyewe mbali na jina na umri wao

Katika hali hii**, msaada kidogo** utahitajika ili angalau kupata taarifa zaidi kutoka kwa washiriki.

Andika swali kwenye vipande vidogo vya karatasi na kuvikunja ili washiriki wasiweze kusoma swali mapema. Baada ya hapo, kila mshiriki anapaswa kuchukua angalau kipande kimoja cha karatasi na kujibu maswali wakati wa mzunguko wa mawasilisho.

Tumia maswali tofautitofauti iwezekanavyo ili maswali machache tu yajirudie. Kwa njia hii washiriki hujifunza mambo mbalimbali kuhusu kila mmoja. Yafuatayo ni mfano wa maswali hayo:

- ✓ Ni sauti gani kubwa zaidi ambayo umewahi kuisikia?
- ✓ Ni tukio gani la mwanzo kabisa wa maisha yako ambalo bado unalikumbuka?
- ✓ Ungependa kuona nini katika kundi hili?
- ✓ Ni uzoefu gani bora ulioupata katika kambi nyingine?
- ✓ Ni eneo gani la kufurahisha zaidi katika filamu ambayo umewahi kuona?
- ✓ Unapenda chakula gani?
- ✓ Unapenda mziki upi?
- ✓ Ni kitu gani bora zaidi umewahi kupitia maishani?
- ✓ Ni daraja gani bora umewahi kupata shuleni na katika somo gani?
- ✓ Ikiwa ungeweza kuwa mtu mwingine, ungependa kuwa nani zaidi?
- ✓ Una jina la utani? Litaje?
- ✓ Ni mwanamziki gani unampenda zaidi?
- ✓ Ni tamthiliya gani ya kila siku katika TV unaipenda ?
- ✓ Nukuu yako ya filamu unayoipenda ni ipi?
- ✓ Ni sehemu zipi umewahi kuishi?
- ✓ Ni vitu gani unapendelea zaidi maishani?
- ✓ Je, unafuga wanyama nyumbani? Taja majina yao?
- ✓ Unapenda zaidi kitabu gani?
- ✓ Unatarajia nini kutoka kwenye semina hii?
- ✓ Kama ungeweza kununua kitu chochote unachotaka (halisi au cha kubuni), ungenunua nini?
- ✓ Unapenda rangi gani?
- ✓ Ni kumbukumbu gani ya utotoni unipenda zaidi?
- ✓ Milima au bahari? Taja sababu?
- ✓ Kitabu au mfululizo wa tamthiliya? Taja sababu?
- ✓ Msimu wa mvua au msimu wa kiangazi? Taja sababu?
- ✓ Je, una kauli mbiu katika maisha? Itaje kama unayo?
- ✓ Ni unafiki ni sehemu gani nzuri zaidi ungetamani kwenda likizo ya mapumziko?
- ✓ Ulizaliwa wapi?

**Njia mbadala / tofauti:** : Ili kutofautisha, maswali mengine yanaweza kuandikwa kwenye bango kubwa au kwenye ubao mweusi mapema. Maswali haya tofauti lazima yajibiwe na washiriki wote

**Tafakari / tathmini / ufuatiliaji / ufafanuzi wa mafundisho:** Hapa, taarifa kuhusu mafundisho, maswali halisi, msukumo wa kutafakari nk. unaweza kutolewa.

**Ikiwa ni lazima kwa zoezi lako vifaa vya kuchapisha:** Unaweza kujumuisha michoro, kadi, karatasi nk. chapisha, kama msaada wa mafundisho.

# Module 1:

# Ufuatiliaji wa utambulisho binafsi na wa pamoja kama kikundi

**4.1. Moduli 1: Kiambata cha utambulisho binafsi na wa pamoja kama kikundi**
**Mbinu za Moduli 1**
**Njia ya 1: Nini kinanifanya niwe nilivyo?**

**Washiriki wanatafakari juu ya maoni yao na thamani yao binafsi**

**Kuanzia umri wa miaka 16 kiwango cha ugumu kinashuka**

**Kufikiria kuhusu vikundi vya maneno na kuandaa ramani za dhana kwa usambazaji**

**Kadri ya dk 45.**

Mbinu inayolenga Lugha:
Haifai kwa watu wasiojua kusoma na kuandika.

**Awamu za warsha: Njia hii inafaa sana kwa awamu ya kuingilia ili kuanganisha kujitafakari.**

**Utaratibu:** Mwanzo, kila mshiriki atapewa karatasi ya kazi namba 1, ambayo atapata dakika 5 za kuisoma na kuelewa kazi, na pia atapata nafasi ya kuuliza maswali. Baadaye, kila mshiriki anapewa dakika 15 za kufikiria yeye mwenyewe kuhusu wasifu wake na kuuandika kwenye karatasi. Iwapo mshiriki anaona vigumu kuelewa kinachohitajika hapa, mapendekezo ya kuchochea mawazo yanaweza kutolewa. Kwa mfano, aina ya wasifu inaweza kutajwa. Baada ya muda kuisha, karatasi ya kazi namba 2 husambazwa kwa washiriki. Hapa pia, washiriki wana dakika 5 kila mmoja kusoma kazi na kuuliza maswali ikiwa ni lazima. Hapa wana dakika nyingine 20 za kufikiria kwa makini uzito wa wasifu wao na kuzingiza kwenye dira ya utambulisho. Ikiwa wanahitaji muda zaidi, ni muhimu kuzingatia hili na kuongeza muda takribani dakika 5-10.

**Tafakari:** Baadaye, matokeo ya washiriki hujadiliwa pamoja katika kikundi. Washiriki watapitia wasifu tofautitofauti na pia uzito tofautitofauti wa washiriki. Hii inachochea ufahamu wa tofauti miongoni mwa kikundi.

## Kutengeneza Ramani ya Fikra (Mindmaping)

Njia hii hutumia karibu uwezo wote wa ubongo wa mwanadamu na kuweza kushughulikia kwa ufanisi na kuona matatizo kwa maneno mafupi..

**Karatasi 1: "Sifa za utambulisho"** Utaelezeaje utambulisho wako? Ni sifa gani zinazokutofautisha na wengine? Ikikubidi ujieleze kwa mgeni, utajielezeaje?

Andika sifa zinazokuja akilini mwako kwenye mistari ya ramani ya fikra..



**Karatasi ya 2: "Rada ya Utambulisho"**

Angalia tena wasifu ulioorodheshwa na jaribu kuuorodhesha kulingana na umuhimu wake. Unafikiria nini, elezea utambulisho wako zaidi na kwa uchache? Panga wasifu wako kwenye rada. Kadiri sifa zinavyozidi kuwa muhimu, ndivyo unavyoziweka katikati ya rada..



[1]

[1](cf. Meinert, Stollt 2009)

**Njia ya 2: Uundaji wa makundi**

**Washiriki wana muhtasari wa vitengo vinavyowezekana na wamehamasika kuvijaza kwa sifa zinazofaa.**

**kwanzia miaka 16**

**Washiriki wote wanahitaji kalaam .kiwango cha ugumu ni cha chini**

**muda unaohitajika kwa njia hii ni makadirio ya dakika 20**

Mbinu inayolenga Lugha: Inahitaji watu wanaojua kusoma na kuandika. Matumizi ya pamoja katika kazi ya kikundi.

**Awamu za warsha: Njia hii inafaa sana kwa awamu ya mwanzo ili kuanganisha vitengo na wasifu na sifa zinazohusiana nazo**

**Utaratibu** : Kila mshiriki anapokea karatasi "makundi ya utambulisho". Sasa ana dakika 5 za kusoma kazi na kufafanua kazi na maswali yanayoweza kuulizwa. Mara tu kila mtu anapoelewa kazi au maswali, wana dakika nyingine kumi za kuainisha masharti katika makundi.

**Tofauti:** Ikiwa washiriki wana mawazo yao wenyewe, upanuzi au mapendekezo ya kuboresha orodha ya makundi, inaweza pia kubadilishwa pamoja darasani washiriki wakipendelea.[2]

[2] (cf. Meinert, Stollt, 2009)

**KARATASI YA KAZI: "AINA ZA VITAMBULISHO" Istilahi ipi ni ya kitengo kipi? Upande wa kushoto kuna kitengo, upande wa kulia, istilahi. Orodhesha istilahi katika katengo kwa kuziunganisha na mstari**

**Aina:**

**Kipindi:**

**Dini:**

**Asili:**

**Jambo alipendalo mtu:**

**Jinsi:**

Rangi ya nywele

kiingereza

kuimba

Rangi ya Nywele

kiurafiki

Mpira wa miguu

Kiislam

Kikristo

**Utambulisho unaathiri vipi maisha ya kila siku?**

**Maandalizi:** Kwa zoezi hili, kwanza kabisa orodha ya washiriki wote wa darasa inagawanywa katika makundi mawili, kisha hali ndogo ya mazungumzo ya kila siku inapaswa kufikiriwa na kuandikwa kwenye karatasi. Kwa mfano, mtu anayeomba mtu amwelekeze njia, yaani anahitaji msaada. Kwa kuongezea, orodha ya wasifu inahitajika kwa watu wote wawili. Kwa mfano, kutoka kwenye makundi:

- ✓ Hisia
- ✓ Dini
- ✓ Asili, n.k.

**Njia ya 3**

Maswali ya miundo na sheria za uraia na kijamii.

Kuanzia miaka 16, kiwango cha ugumu ni cha kati. Kazi ya ushirika kwa watu 2 kila kikundi.

Kalamu

Inachukua karibia dakika 35.

**Awamu za warsha: Awamu yenye matatizo (Problematizing phase)**

**Utaratibu:** : Washiriki hupokea karatasi "Mchakato wa Mazungumzo", ambayo uigizwaji wa mazungumzo kati ya watu wawili unafanywa. Kwanza kabisa, washiriki wanagawanyika katika makundi yaliyofikiriwa hapo awali, kisha kila mdau anapewa mtu kutoka kwenye karatasi kupitia namba 1 na 2. Kisha washiriki hupewa fursa ya kusoma zoezi hilo na kufafanua maswali yoyote ambayo wanaweza kuwa nayo. Wanapaswa kupewa kama dakika 5 kufanya hili zoezi. Mara baada ya kila mshiriki kulielewa zoezi, wadau hao wawili husoma sehemu zao za maandishi kwa sauti kwa kila mmoja. Sasa wadau wanafikiria ni wasifu upi wa mtu mwingine aliyeorodheshwa hapa chini unaonekana kuwa muhimu kwao kwa mazungumzo, na wanazungushia neno husika kwa kalamu ya chaguo lao. Washiriki wanapaswa kupewa dakika 25 kusoma na kuweka alama kwenye wasifu muhimu.

**Tafakari** : Timu zote zinapomaliza, matokeo ya washiriki hujadiliwa kwa pamoja darasani. Kutakuwa na kuchepukachepuka kutoka maoni ya jumla, kwani zoezi hili daima huzingatiwa kwa malengo. Washiriki ambao matokeo yao yanatofautiana na maoni ya jumla wanapewa nafasi ya kuhalalisha uamuzi wao na hivyo kutoa

pendekezo jipya la kuchochea mawazo kwa darasa au kuchochea duru ya majadiliano. [3]

**Karatasi 1: "Mtiririko wa mazungumzo "**

A Mtogo" amesafiri kwenda "Ghana" kwa likizo na anataka kuuliza mtaani kuhusu njia inayoelekea katika "kituo cha mabasi" kinachofuata. Ili kufanya hivyo, anamuuliza mwenyeji.

Kwanza kabisa, soma sehemu ya mazungumzo kati ya watu hao wawili. Kisha zingatia wasifu wanaohusishwa nao. Kutokana na hali ya mazungumzo unadhani ni wasifu upi muhimu? Zungushia duara kwenye wasifu muhimu..

[3] (Diaconu 2008, p.60 ff.)




| **Tabia 1:** | **Tabia 2:** |
|---|---|
| mwembamba | husaidia |
| Mkristo | ana urafiki |
| Mwalimu wa shule ya awali | anaongea lugha zaidi ya moja |
| Mfaransa | mpiga gitaa |
| Anapenda kusafiri | dereva teksi |

**Njia ya 4: Mkutano wa Utambulisho**

**Washiriki wanaona kwa njia ya vitendo umuhimu wa sifa za utambulishokwa mazingira yao.**

**Kuanzia takriban miaka 16: Kiwango cha utata kinaelezewa kama maana.**

**Saizi ya kikundi ni watu 5**

**Mabango 3 na kalamu zinahitajika kwa njia hii.**

**Takriban dakika 65**

Mbinu ya kutumia lugha/maneno: Inafaa

**Awamu za warsha: Awamu za kujifunza.**

**Maandalizi** Kwa njia hii ni muhimu kuwapa washiriki uzoefu kwa vitendo. Kwa hili, inasaidia kuwapa washiriki mazingira ya majadiliano kupitia samani na mapambo. Andaa chumba kwa kuweka meza 3 zenye viti vya kutosha kuzunguka chumba. Pandezesha meza, mfano kwa kitambaa. Fikiria viongozi watatu wa kundi ambao watakaa katika moja ya meza tatu wakati wa igizo. Kila meza itakuwa na kadi za meza 4 zenye wasifu tofauti juu yake. Mfano wa sifa za Kwenye Makundi:

- ✓ Dini
- ✓ Mwonekano
- ✓ Hisia

**Utaratibu** Mwanzoni , viongozi wa makundi huwekwa kwenye meza tatu na kiongozi mmoja huteuliwa kwa kila kikundi. Kila mmoja wa viongozi wa kila kikundi hupokea bango na kalamu. Sasa mazingira ambayo zoezi linafanyika yanajadiliwa na viongozi wa kikundi na maswali yanayoweza kuulizwa. Timu ya semina inafafanua kuwa huu ni mjadala wa kikundi sawa na mazungumzo kati ya marafiki katika meza ya duara. Kila mshiriki anachukua jukumu alilopewa kwenye kadi zilizopo mezani. Majukumu haya yanawakilisha wasifu binafsi binafsi na ubora. Baada ya dakika 20, kila mshiriki hubadilisha meza na pia wasifu binafsi. Ni viongozi wa kikundi pekee ambao wanabiki

wameketi na kuwajulisha wanakikundi wafuatao kuhusu mjadala na yaliyojiri. Ili kupitisha mjadala kwa wanakikundi wajao kwa njia bora zaidi, kiongozi wa kikundi anarekodi dondoo muhimu zaidi kwenye mabango kulingana na wasifu. Kwa jumla, washiriki hubadilisha meza mara mbili ili kila mtu akae katika kila meza mara moja. Aidha, timu ya warsha inaeleza sheria za majadiliano ili majadiliano yaendeshwe kwa utulivu.

**Tafakari** Mwisho, maudhui yaliyofupishwa ya majadiliano yatawasilishwa na viongozi wa kikundi. Mabango yataonesha tofauti ambazo zitajadiliwa kwa jumla..

**Tofauti** Kunaweza kuwa na tofauti katika utekelezaji kwa kugawa swali linaloongoza kwa kila meza. Inawezekana pia kufanya bila kiongozi wa kikundi, ili kila mwanakikundi wa meza abadilishwe katika makundi yaliyotangulia. Pia, sifa za wasifu zinaweza kurekebishwa kwa watu badala ya kubadilika..[4]

**Ushawishi**

Baadaye, siku nzima inapaswa kuandikwa au kuchorwa. Baadaye, matokeo hujadiliwa katika kundi hilo. Baadaye, wale wanaofikiria wanapaswa kutafakari yaliyojiri na kipi ni muhimu sana kwao na ni kipi kati ya hizi kinaweza kuwa lengo kwao. Wakati huo huo, wanaweza kuzungumza juu ya nini kinaweza kufanywa ili kufikia malengo haya katika siku zijazo.[43]

**Kufuatilia:**

Baada ya majaribio ya mawazo kufanywa na kujadiliwa, washiriki wanapaswa kuamua wenyewe ni vipengele gani vya majaribio ya mawazo ni muhimu kwao na kile wanachotaka kufikia. Kuhusu jaribio la pili la mawazo, wanapaswa kutofautisha kama haya ni malengo muhimu kwao au shughuli ambazo tayari wanafanya mara kwa mara na kwamba wanafurahia, ambapo shughuli za burudani pia zinaweza kuwa lengo.

[43] cf. (Münster, 2021)

# Moduli 4:

# Kuambatana na Kujitolea kwa Jamii

### 4.4. Module 4: Kuambatana na Kujitolea kwa Jamii

Uendelevu unaelezewa kwa undani zaidi na malengo ya "Elimu kwa Maendeleo Endelevu" (ESD). Mwaka 2015, malengo 17 ya "Elimu kwa Maendeleo Endelevu" yalipitishwa katika kilele cha mkutano wa Umoja wa Mataifa. Jumla ya Maitaifa 193 yalipiga kura kutekeleza malengo hayo. Waliahidi kuzingatia mkataba huu wa "Global Future Treaty" ifikapo mwaka 2030 na kuhakikisha maisha ya heshima kwa watu wote duniani (taz. O.A. (O.J.) a). Masuala ya binadamu kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, njaa, umaskini na uhamiaji, ni miongoni mwa mada ambazo zimepata umuhimu mkubwa na ambazo zinapaswa kushughulikiwa kupitia malengo ya ESD (taz. ebd.). Uendelevu sio tu kwa uhifadhi wa asili na ulinzi wa mazingira, lakini ni juu ya mitazamo ya kimataifa ya kuishi pamoja. Zaidi ya yote, mustakabali wa vizazi vijavyo unapaswa kuzingatiwa ili kuwaleta karibu na ulimwengu ambao kila mtu anaweza kuishi kwa heshima (tazama Kühnert, T. (Septemba 16, 2019)). Ili kufanikisha hili, vizazi hivi lazima vielimishwe juu ya mambo ya uendelevu, malengo ya ESD na yaliyomo ndani yake. Malengo si maudhui ya moja kwa moja kisiasa, bali ni mada ambazo mtu hukutana nazo katika maisha ya kila siku na hivyo kuwa na umuhimu kwa kila mtu. Kwa sababu hii, malengo ya mtu binafsi yatashughulikiwa kwa undani zaidi, pamoja na kuwasilishwa kwa utaratibu kiundani, ili yatolewe ipasavyo. Katika maudhui yafuatayo, si malengo yote yatarejewa, ila baadhi yamechaguliwa ambayo yanapaswa kuzingatiwa, mfano jinsi uchafuzi wa mazingira yetu kupitia matumizi makubwa ya bidhaa za plastiki unaweza kupunguzwa kwa kuzitumia plastiki hizohizo kuzalisha tena bidhaa. Aidha, baadhi ya njia hizi pia zinaweza kubadilishwa ili ziweze pia kuwa na manufaa kwa maudhui ya malengo yasiyotengwa. Ikumbukwe pia kwamba malengo huwasilishwa hapa tofauti na kila moja na yanathibitishwa kwa njia. Hata hivyo, malengo yanapaswa kuonekana katika hali ya kuhusiana.

**Mbinu za Moduli ya 4**
**Njia ya 1: Tunahitaji kiasi gani?**

Kupanua maarifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kutengeneza mikakati ya utatuzi wa matatizo na fikra makini. Kukuza mshikamano na motisha ya kutatua matatizo ya kimataifa.

Kuanzia umri wa miaka 14. Ukubwa wa kikundi ni washiriki 5-6 kila mmoja. Kiwango cha utata kinaelezwa.

Mfano wa pesa (za kucheza), chati mgeuzo, kalamu, nakala
za Malengo ya Uendelevu kwa kila kikundi

Takribani dakika 15 - 20

Mbinu inayozingatia lugha: inafaa kwa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika. Wagawe vikundi kwa njia ambayo wasiojua kusoma na kuandika wanaweza kusaidiwa.

**Awamu za warsha: Mbinu inaweza kutumika ama katika awamu ya kuanzia au na mada zilizotengenezwa hapo awali katika awamu ya chelezo.**

**Utaratibu:**

1. Kiongozi wa mafunzo anawauliza washiriki wanajua nini kuhusu SDGs. Je, washiriki wanaweza kuorodhesha SDG ngapi?
2. Kisha SDGs huwasilishwa kwa msaada wa bango. Inapaswa kuwekwa wazi kuwa ufadhili wa nje ni kipengele kimoja tu kati ya vingi, na kwamba SDGs pia zinahusu maendeleo ya uwezo, biashara na masuala ya kimfumo. Hata hivyo, zoezi hili linaangazia suala la ufadhili.
3. Vikundi vidogo vidogo vyenye watu watano hadi sita vinaundwa. Mfano kuhusu hali ifuatayo inatolewa: Ingawa wataalam wa kifedha wamejitahidi kupata fedha kwa SDGs, bado kuna pengo la ufadhili. Vikundi vidogo vinawakilisha vikundi-kazi vya Umoja wa Mataifa ambavyo vinatakiwa kutathmini ikiwa dola bilioni 1750 za Marekani kwa mwaka zinatosha kufikia lengo la 2 (hakuna njaa), Lengo la 3 (huduma bora za afya), Lengo la 4 (elimu bora) na Lengo la 6 (maji safi na usafi wa mazingira). Ili kuweka uelewa zaidi kuhusu kiasi cha dola bilioni 1750 angalau kwa kiasi fulani, washiriki wanapewa taarifa kwamba pato la dunia (GDP) mwaka 2014 lilikuwa dola bilioni 77,000. Pato la Taifa la Marekani mwaka 2014 lilikuwa

dola bilioni 17,500; la Ujerumani, dola bilioni 3,850; la Somalia, dola bilioni 5.7; na la Togo, dola bilioni 4.575

> Pato la Taifa (GDP) ni kipimo cha utendaji wa uchumi katika kipindi fulani. Inapima thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa kitaifa.
>
> *chanzo:* *https://www.destatis.de/DE/Themen/Wirtschaft/Volkswirtschaftliche-Gesamtrechnungen-Inlandsprodukt/Methoden/bip.html*

4. Washiriki wanaelezwa kuwa pesa 1 za kuchezea ni sawa na dola bilioni 1, hivyo washiriki wanaweza kutumia hadi dola bilioni 1,500 ikiwa wataona kuna haja ya kufanya hivyo.
5. Vikundi vidogo vijadili SDGs na kukadiria ni kiasi gani kingepaswa kutengwa kwa kila lengo.
6. Fedha zinazotolewa sasa zinawekwa kwenye kadi lengwa. Washiriki hawapaswi kutumia pesa zote - SDGs 13 zilizobaki hakika pia zitahitaji kuongezwa zaidi.
7. Halafu vikundi vinaripoti kwa upande wake ni kiasi gani cha fedha walichotenga kwa kila lengo na kuweka kiasi kwenye chati. Hakupaswi kuwa na mjadala katika hatua hii; ila kutakua na majadiliano ya jumla hapo badaye. Inatosha kwa msimamizi kuchochea umakini wa washiriki katika tofauti zilizopo kwenye kazi zao.
8. Washiriki wanaambiwa ni kiasi gani cha ziada kilikadiriwa na taasisi ya utafiti ya Uingereza ODI:

> Target 2: $50 billion
>
> Target 3: $40 billion
>
> Target 4: $40 billion

9. Kila makadirio yanarekodiwa kwenye chati kila kikundi na kalamu ya rangi tofauti na vikundi hivyo vinatakiwa kupanga upya noti zao ipasavyo na kuhesabu kiasi cha fedha kilichobaki.
10. Hata hivyo, dola bilioni 1750 ambazo zinapatikana hazitoki hewani; kiasi hiki kinalingana na matumizi ya kijeshi duniani (Stand 2017).

**Tafakari:** Kwanza kabisa, wanatathmini jinsi zoezi lilivyokwenda na kisha kuzungumzia uzoefu wa kujifunza kwa kuuliza maswali yafuatayo:

- -Kazi ya Makundi ilikuwaje? Je, ilikuwa rahisi kukubaliana kuhusu vipaumbele na makadirio? Kutokubaliana kulitatuliwa vipi?
- Je, kulikuwa na maoni yoyote kuhusu michango inayohitajika kutumia pengo la ufadhili wa SDGs?
- -Vipi kuhusu fedha za ziada zinazohitaji kupatikana kwa malengo mengine 13? Je, washiriki watatumia zaidi ya dola bilioni 1580 zilizosalia kwa ajili hiyo?
- Bila shaka usalama ni kitu muhimu sana. Ni vitisho gani vikubwa kwa usalama wa binadamu leo, ndani ya nchi na duniani kwa ujumla?
- Unafikiri shilingi bilioni 1750 zinazotumika kwa matumizi ya kijeshi leo zingetumikaje kwa busara zaidi?
- -Ni haki zipi za binadamu ambazo ni muhimu kwa lengo la SDG 16, Amani na Haki? Na kwa malengo 2,3,4 na 6?
- Kikundi kinaweza kufanya nini katika ngazi ya mitaa na kitaifa kusaidia SDGs?

**Tofauti**: Zoezi pia linaweza kufanywa kama igizo kujadili bajeti ya silaha na SDGs. Makundi hayo yamepewa majukumu tofauti, kwa mfano maafisa wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoshughulikia umaskini, VVU au elimu, wasemaji wa sekta ya silaha, mwanachama wa chama cha wafanyakazi katika sekta ya silaha, wanajeshi na wadau wengine. Kila jukumu linahitaji miongozo michache, kwa mfano:

Serikali: Kipaumbele chako ni kuboresha hali ya maisha ya watu wako, lakini pia usalama wa nchi yako.

Mashirika yasiyo ya kiserikali: Kipaumbele chako ni kupunguza kwa kiasi kikubwa bajeti za silaha na kupunguzwa kwa madeni kwa nchi maskini zaidi.

Sekta ya silaha: Kipaumbele chao ni kuhifadhi masoko na faida yako, lakini wako tayari kujadiliana.

Chama cha wafanyakazi wa sekta ya silaha: Kipaumbele chao ni maisha bora kwa amani, lakini pia wanaogopa kupoteza kazi zako.

**Nyenzo za habari: SDG 2,3,4 & 6**

Malengo Yote ya Maendeleo Endelevu yamegawanywa katika vichwa vidogo vya malengo, na kila lengo dogo litafikiwa kwa tarehe fulani. Malengo madogo kama Malengo 2 (Hakuna Njaa), 3 (Afya na Ustawi), 4 (Elimu ya Ubora) na 6 (Maji Safi na Usafi wa Mazingira) yameorodheshwa hapa chini, kwa kua ni muhimu pia kwa mbinu iliyo hapo juu. Muhtasari wa malengo yote unaweza kupatikana kwenye bango, na habari zaidi inaweza kupatikana kwenye ukurasa wa BMZ.

- **SDG 2**:
- **2.1:** Ifikapo mwaka 2030, kukomesha njaa na kuhakikisha kuwa watu wote, • hasa maskini na watu walio katika mazingira hatarishi, wakiwemo watoto wadogo, wanapata chakula salama, chenye lishe na cha kutosha mwaka mzima.
- **2.2:** Kukomesha aina zote za utapiamlo ifikapo 2030, kwa kufikia malengo yaliyokubaliwa kimataifa juu ya kudorora kwa ukuaji na utapiamlo wa watoto walio chini ya umri wa miaka 5 ifikapo 2025 na kuzingatia mahitaji ya lishe ya wasichana balehe, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha na wazee.
- **2.3:** Ifikapo mwaka 2030, tija ya kilimo na mapato ya wakulima wadogo iongezeke maradufu, hususan wanawake, wenyeji, wakulima wadogo, wafugaji na wavuvi, kupitia upatikanaji wa ardhi kwa usalama na usawa, rasilimali nyingine za uzalishaji na pembejeo, maarifa, huduma za kifedha; masoko, na fursa za kuongeza thamani na ajira nje ya mashamba.
- **2.4:** Ifikapo mwaka 2030, hakikisha uendelevu wa mifumo ya uzalishaji wa chakula na kufuata kanuni za kilimo zinazoweza kuongeza tija na mavuno, kuchangia uhifadhi wa mazingira, kuongeza uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hali mbaya ya hewa, ukame, mafuriko na majanga mengine, na kuboresha ardhi hatua kwa hatua. na ubora wa udongo.
- **2.5:** Ifikapo mwaka 2020, kuhifadhi uanuwai wa kinasaba wa mbegu, mazao, mifugo na wanyama wa kufugwa na jamaa zao wa porini, kupitia benki za mbegu na mimea zinazosimamiwa vyema katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa na kukuza upatikanaji wa manufaa ya matumizi ya rasilimali za kijenetiki na maarifa ya jadi yanayohusiana na ugawaji sawia na sawa wa faida hizo, kama ilivyokubaliwa katika kiwango cha kimataifa.

**SDG 4**

- **4.1:** Ifikapo mwaka 2030, kuhakikisha kuwa wasichana na wavulana wote wanamaliza kwa usawa elimu ya msingi na sekondari bila malipo ambayo inaleta matokeo yanayoweza kutumika na yenye ufanisi.
- **4.2:** Kufikia 2030, kuhakikisha kwamba wasichana na wavulana wote wanapata elimu bora ya utotoni, matunzo na elimu ya awali wanayohitaji ili kutayarishwa kwa shule ya msingi.
- **4.3:** Ifikapo mwaka wa 2030, hakikisha upatikanaji sawa kwa wanawake na wanaume wote kwa elimu ya ufundi, ufundi na elimu ya juu kwa bei nafuu na bora, ikijumuisha masomo ya chuo kikuu.
- **4.4:** Ifikapo mwaka 2030, kuongeza kwa kiasi kikubwa idadi ya vijana na watu wazima walio na sifa stahiki, ikiwa ni pamoja na sifa za kiufundi na ufundi, kwa ajili ya kuajiriwa, kazi zenye staha na ujasiriamali.
- **4.5:** Kufikia 2030, kuondoa tofauti za kijinsia katika elimu na kuhakikisha upatikanaji sawa wa ngazi zote za elimu na mafunzo kwa watu walio katika mazingira magumu katika jamii, yaani watu wenye ulemavu, wenyeji na watoto walio katika mazingira hatarishi.
- **4.6:** Kufikia 2030, hakikisha kwamba vijana wote na idadi kubwa ya watu wazima wa kiume na wa kike wanajifunza kusoma, kuandika na kukokotoa.
- **4.7**: Ifikapo mwaka 2030, hakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata ujuzi na sifa zinazohitajika ili kukuza maendeleo endelevu, ikiwa ni pamoja na kupitia elimu kwa maendeleo endelevu na maisha endelevu, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, utamaduni wa amani na kutokuwa na vurugu, uraia wa kimataifa na kuthamini tofauti za kitamaduni na mchango wa utamaduni katika maendeleo endelevu.

**SDG 6**

- **6.1:** Kufikia upatikanaji wa maji safi na salama ya kunywa kwa wote hadi mwaka wa 2030 kwa wote na kwa bei nafuu.
- **6.2:** Ifikapo 2030, kufikia upatikanaji wa vyoo na usafi wa kutosha na wa usawa kwa wote na kukomesha ufukara kupitia ujenzi wa nje, kwa kuzingatia maalum mahitaji ya wanawake. na wasichana na watu walio katika mazingira magumu.
- **6.3:** Kufikia 2030, kuboresha ubora wa maji kwa kupunguza uchafuzi wa mazingira, kukomesha utokaji na kupunguza utolewaji wa kemikali na dutu hatari, kupunguza nusu ya idadi ya maji machafu ambayo hayajatibiwa, na kuongeza kwa kiasi kikubwa kuchakata na kutumia tena yakiwa safi na salama duniani kote.
- **6.4:** Ifikapo mwaka 2030, kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji katika sekta zote na kuhakikisha unywaji endelevu na usambazaji wa maji safi ili kukabiliana na uhaba wa maji na kupunguza idadi ya watu wanaokabiliwa na uhaba wa maji.
- **6.5:** Ifikapo mwaka 2030, kutekeleza usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji katika ngazi zote, ikijumuisha kupitia ushirikiano wa kuvuka mipaka inapobidi.
- **6.6:** Kufikia 2020, linda na kurejesha mifumo ikolojia iliyounganishwa na maji, ikijumuisha milima, misitu, ardhi oevu, mito, vyanzo vya maji na maziwa.

**Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu (SDGs)**

1. Kumaliza umaskini kwa namna zake zote na kila mahali;
2. Kukomesha njaa, kufikia usalama wa chakula na kuboresha lishe, na kukuza kilimo endelevu;
3. Kuhakikisha maisha bora kwa watu wote wa rika zote na kukuza ustawi wao;
4. Kuhakikisha elimu jumuishi, yenye usawa na ubora na kukuza fursa za kujifunza kwa wote (Kazi ya Academie Bilimon ina lengo hili);
5. Kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji kwa wanawake na wasichana wote (Kazi ya Academie Bilimon pia ina lengo hili);
6. Kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa maji na usafi wa mazingira kwa wote;
7. Kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, ya uhakika, endelevu na kwa wakati kwa wote;
8. Kukuza ukuaji wa uchumi endelevu, jumuishi na endelevu, ajira zenye tija zenye tija na kazi nzuri kwa wote;
9. Kujenga miundombinu imara, kukuza viwanda jumuishi na endelevu na kusaidia ubunifu;
10. Kupunguza ukosefu wa usawa ndani na kati ya majimbo (Kazi ya Academie Bilimon pia ina lengo hili);
11. Kufanya miji na makazi kuwa jumuishi, salama, stahimilivu na endelevu;
12. Kuhakikisha matumizi na uzalishaji endelevu;
13. Kuchukua hatua za haraka kupambana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake;
14. Kuhifadhi na kutumia bahari, rasilimali za baharini kwa ufanisi kwa maendeleo endelevu;
15. Kulinda, kurejesha na kuendeleza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya ardhi, kusimamia misitu endelevu, kupambana na jangwa, kusimamisha na kurekebisha uharibifu wa udongo na kuzuia upotevu wa viumbe hai;
16. Kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu, kutoa fursa ya upatikanaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye ufanisi, uwajibikaji na jumuishi katika ngazi zote (Kazi ya Academie Bilimon pia ina lengo hili);
17. Kuimarisha njia za utekelezaji na kufufua ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo endelevu (Kazi ya Academie Bilimon pia ina lengo hili).

**Usawa wa Kijinsia:**

Lengo la usawa wa kijinsia ni kufikia haki na uwezeshaji kwa wanawake na wasichana wote.

***Chanzo**: cf.* *https://www.unesco.de/bildung/agenda-bildung-*

**Njia ya 2: Picha nyingine ya kioo**

**Maandalizi:** Upatikanaji wa vifaa, kukaa katika duara

**Maelezo:** Washiriki hufikiria juu ya mila potofu za kijinsia na kuziita katika swali..

Ukuzaji wa ufahamu kwa dhana potofu. Tambua haki zisizo sawa kati ya watu na zijadili kwa umakini

Kuanzia takriban miaka 14. Kiwango cha utata kinakadiriwa kuwa kutoka kati hadi ngumu. Idadi ya washiriki inapaswa kuwa watu 5-20.

Hadithi mbili, kadi zilizo gundi

Dakika30 hadi 60

Mbinu inayolenga lugha: inafaa kwa watu wasiojua kusoma na kuandika

**Awamu za warsha: Majadiliano ya kikundi kuhusu SGDs 5,10,16**

**Utaratibu:**

Washiriki watasikiliza hadithi fupi, lakini hawapaswi kuzungumza au kuwasiliana kwa njia nyingine yoyote wakati wa kusoma (kwa mfano kupitia mawasiliano ya macho ya kazi). Katika duara lililokaa, inasaidia ikiwa washiriki watafumba macho wakati wa kusikiliza..

**1.** Washiriki wanafahamishwa kuwa watalazimika kusikiliza hadithi mbili zijazo.

2. Kiongozi anasoma hadithi mbili. Katika kipindi hiki washiriki wakisikiliza bila kutoa maoni.

3. Baada ya kusoma, washiriki wanaruhusiwa kujadili kwa kifupi kile walichokiona. Mjadala unapaswa kuwa mfupi iwezekanavyo na usiingie kwa undani sana. Hii inalenga kuleta mvuto wa kwanza wa juu juu.

4. Sasa hadithi zote mbili zinasomwa tena. Wakati huu, hata hivyo, polepole kidogo, kwani washiriki sasa wana uwezekano wa kuita "kukatisha" mara tu wanapoona ubaguzi wa kijinsia. Hili litajwa na mshiriki husika na kubainishwa na mkuu wa warsha kwa wote kuona..

**Tafakari:**

Mara baada ya mila potofu zote kupatikana, kundi linaweza likaanza mjadala. Hapa msimamizi anachukua dhana moja potofu baada ya nyingine na kuuliza maswali:

a. Kwa nini kuna mila potofu?

b. Je, mila hii potofu bado inafaa?

c. Je, mila hii potofu inahalalishwa?

d. Je, tunataka kuendeleza mila hii potofu

**Kiboksi cha taarifa: Ubaguzi**

Ubaguzi ni sifa zinazohusishwa na kundi la watu wenye sifa sawa au zinazofanana. Kwa kawaida, ubaguzi hautegemei ushahidi, na ikiwa upo, unatokana na ushahidi mdogo. Ubaguzi umejikita katika jamii na ni vigumu kubadilika. Kwa mfano, katika malengo ya usawa wa kijinsia, mila ubaguzi unaweza kumaanisha kwamba wasichana mara nyingi hupewa sifa ya "kihisia sana", lakini pia kuna wasichana wengi ambao hawana hisia sana na, kinyume chake, wavulana wanaweza pia kuwa na hisia sana.

*Chanzo: cf. Giddens, Anthony and Phillip W. Sutton (2017): Sociology, eighth edition. Polity Press, Cambridge, p. 1016*

**Njia ya 3: „ Ninachotaka na kile ninachofanya**

Kuvumbua vipaji na maarifa ya mtu mwenyewe na yale ya wengine. Kutambua athari za ubaguzi wa majukumu ya kijinsia.

Kuanzia takribani miaka 14-18.
Ukubwa wa kikundi takribani watu. 8-20.

Na ikiwezekana kalamu na karatasi
Nakala ya utafiti

Muda unaohitajika ni dakika 45

Mbinu inayozingatia uandishi: Haifai kwa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika. Hata hivyo, hii inaweza kuainishwa katika vikundi ili kila kikundi kiwe na mshiriki au kiongozi anayeweza kuandika sentensi.

**Awamu za semina: Mijadala ya vikundi na kujitafakari na inajumuisha SDGs 5,10,16**

**Utaratibu:**

**Maandalizi:** Ikiwezekana toa nakala ya utafiti.

**Maelezo:** Watoto wanasema kile wanachopenda kufanya, kile ambacho hawapendi kufanya au kile ambacho wangependa kufanya lakini ambacho kinachukuliwa kuwa "kisichofaa" au " si cha jinsia yao. Wanazungumzia mila potofu za kijinsia na kufanya uhusiano na haki za binadamu

1. Ili kuanzisha mada, mkufunzi anauliza kikundi maswali yafuatayo: Je, kuna tabia na vitendo vinavyochukuliwa ni vya wasichana " tu au "vya wavulana" tu? Ikiwezekana, washiriki wanapaswa pia kutoa mifano halisi.
2. Sasa kila mshiriki anapata kalamu na karatasi au, ikiwezekana, dodoso lililofungwa kujibu maswali yafuatayo.

- Orodhesha mambo manne unayofanya na yanayokufanya kuwa, ambayo unayapenda na yanayosemekana kuwa "sahihi kwa jinsia yako".
- Orodhesha vitu vinne unavyofanya au vinavyokufanya ushikamane ambavyo huvipendi na ambavyo vinasemekana kuwa "sahihi kwa jinsia yako".
- Orodhesha vitu vinne ambavyo hufanyi au unavyo ambavyo pia huvipendi na vinasemekana kuwa "sawa kwa jinsia tofauti".
- Orodhesha vitu vinne ambavyo hufanyi au huna ambavyo unapenda kweli ambavyo vinasemekana kuwa "sawa kwa jinsia tofauti"".

Kiongozi wa semina anabainisha mambo yanayotajwa mara kwa mara au yanayojirudia mara kwa mara katika karatasi, ambayo yatarudishwa tena kwa raundi ya tafakari. Karatasi inaweza kuonekana hivi:

| | Ninachopenda kufanya na kinachonifanya kuwa wa kipekee, kile ninachopenda na wanachosema ni "kizuri kwa jinsia yangu" | Ninachopenda kufanya na kinachonifanya niwe wa kipekee,, Kitu ambacho sipendi, ingawa wanasema ni "kizuri kwa jinsia yangu " | Ninachopenda kufanya na kinachonifanya kuwa maalum,, Ninachopenda, na ingawa wanasema ni "kizuri kwa jinsia tofauti" " | Kile ambacho sipendi kufanya na kile ambacho sina, ambacho kinamaanisha kuwa ni "kizuri kwa jinsia tofauti" |
|---|---|---|---|---|
| Wavulana | | | | |
| Wasichana | | | | |

Wajibu wa kijinsi:

Wajibu wa kijinsi mara kadhaa huwa na uhusiano wa kitamaduni wa nchi kwa hiyo huwa tofauti. Hata kama huweka kikomo kwenye ushiriki wa wanawake

**Tafakari:**

1 Uliza maswali yafuatayo kwa ufuatiliaji, kwa mfano:

a. Ni wapi ulishangazwa na mambo fulani ambayo washiriki wengine waliyataja?

b. Unapoangalia orodha ya vitu ambavyo washiriki wanapenda au wangependa kufanya hapa lakini hawakuweza kufanya, je, unaona namna?

c. Nini kinatokea kwa msichana ambaye "ana tabia kama mvulana"? Nini kinatokea kwa mvulana ambaye ana tabia "kama msichana"? Kwa nini hii inatokea?

d. Je, wanafamilia wako wana mawazo sawa kuhusu "haki" kwa wanaume na wavulana au kwa wanawake na wasichana?

e. Je, unafikiri mawazo haya ya "haki" kwa wanaume na wavulana au kwa wanawake na wasichana yanatoka wapi?

2. Husisha shughuli na haki za binadamu, kwa mfano kwa kuuliza maswali yafuatayo:

a. Vikwazo dhidi ya tabia za wavulana na wasichana vinaathiri vipi watu binafsi? Wanawezaje kuathiri familia? Na kwenye jamii?

b. Unadhani majukumu ya kijinsia (au mila potofu) yanabadilika kwa sasa? Kama ndiyo, kivipi?

c. Je, umewahi kujaribu kujitetea dhidi ya majukumu ya kijinsia au mila potofu? Nini kilitokea?

d. Kwa nini haki za binadamu za mtu zinapunguzwa na majukumu ya kijinsia/ mila potofu?

e. Tunawezaje kujitetea dhidi ya majukumu ya kijinsia katika kikundi chetu?

**Ushiriki:**

Kushiriki kunamaanisha kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yako mwenyewe, kutumia fursa, kuhusika na kushiriki. Uwezeshaji na ushiriki umeunganishwa (tazama: taswira nyingine ya kioo, kutafakari: "uwezeshaji") na kushiriki malengo sawa kwa kiasi kikubwa.

***Chanzo**: cf. Schönhuth, Michael und Maja Tabea Jerrentrup (2019). Partizipation und nachhaltige Entwicklung. Ein Überblick. Springer VS, Trier, p. 1*

**Utafiti:**

Jina: ____________ Ngono: ________________

| | |
|---|---|
| Ninachopenda kufanya na kinachonifanya kuwa wa kipekee, kile ninachopenda na wanachosema ni "kizuri kwa jinsia yangu ". | |
| Ninachopenda kufanya na kinachonifanya niwe wa kipekee,<br>Kile ambacho sipendi, ingawa wanasema ni "kizuri kwa jinsia yangu" " | |
| Ninachopenda kufanya na kinachonifanya niwe wa kipekee,<br>Ninachopenda, na ingawa wanasema ni "kizuri kwa jinsia tofauti" " | |
| Kile ambacho sipendi kufanya na kile ambacho sina, ambacho inamaanisha kuwa ni "kizuri kwa jinsia tofauti " | |

.

**Njia ya 4: I—(Mimi) Maelezo**

Ukuzaji wa huruma, ubunifu, uvumilivu, uwazi na uchunguzi wa kina wa fani tofauti za masomo.

Kuanzia miaka 14-18. Inapendekezwa kikundi cha watu 4-20. Kiwango cha utata kinakadiriwa kuwa kigumu.

Picha au video fupi kuhusu mada ya matumizi na uzalishaji endelevu

Takribani dakika 60 au zaidi

Mbinu inayolenga lugha: Inafaa kwa watu wasiojua kusoma na kuandika ikiwa kadi zinasomwa kwa sauti mwanzoni. Vinginevyo, ishara zinaweza kutumika

**Awamu za warsha: Awamu ya kutambua matatizo/tathmini**

**Maandalizi:** Uteuzi wa picha na kiongozi wa semina

**Maelezo:** Washiriki hujiweka katika viatu vya mtu kwenye picha na kuandika kwa mtazamo wa mtu huyo.

**Utaratibu:**

Katika kikao hicho, picha imewasilishwa na kiongozi wa semina. Baada ya hapo, yaliyomo kwenye picha hii yanajadiliwa na kundi zima na maswali yanayowezekana yanafafanuliwa. Ni muhimu kwamba ujumbe wa msingi wa picha unajulikana kwa kila mshiriki. Baada ya kikao hiki cha pamoja, washiriki huenda katika kazi za kibinafsi. Kila mshiriki sasa yuko huru kuandika maandishi ya ("I") Mimi…… kuhusu mtu kwenye picha. Haijalishi kama wanachagua mtu ambaye amechapishwa mbele ya picha au ikiwa watachagua mtu ambaye si mhusika mkuu wa picha na anaonekana kana kwamba yuko mbali na picha hafanyi jambo lolote. Kwa picha ambapo msitu unakatwa, washiriki wanaweza ama kujiweka mahali pa mtu anayepinga hilo, mtu anayetekeleza agizo hilo, au hata mteja, ilimradi watu wote wanaoneshwe. Kwa namna nyingine, ingewezekana kuandika kwa mtazamo wa mnyama au hata mti.

Washiriki sasa wanaandika maandishi ya Mimi ("I")…. kwa mtazamo wa mtu aliyechaguliwa. Hii inaweza kuchukua aina nyingi tofauti, kama vile barua ambayo mtu

anaandika, monologia ambayo mtu anatoa au hata shajara. Aina ya uandishi ni suala la washiriki wenyewe kuamua; Inategemea kile wanachofikiria, ni nini kinachoweza kumfaa mtu aliyechaguliwa. Katika “Mimi/I”… jambo la msingi ni kutafakari hali kwenye picha, lakini pia kujiweka mahali pa mtu mwingine. Maswali yafuatayo yanaweza kusaidia katika kuunda maandishi ya Mimi (“I” )

Unafanya nini katika hali ya kwenye picha?

Uliingiaje katika hali hiyo?

Unajisikiaje katika hali hiyo?

Unafikiria nini?

Je, Hali kwenye picha inawezaje kuwa na athari kwa maisha yako ya baadaye?

**Tafakari:**

Tathmini ya njia hii hufanyika tena katika mkutano. Washiriki wakiwasilisha matokeo yao kwa kikundi na kisha kuzungumzia maoni yao. Ni muhimu kusiwe na mitazamo sahihi au isiyo sahihi. Ni hisia za chini ambazo huja kwa njia ya maandishi ya Mimi…, na hizi hazipaswi kutathminiwa. Kwa kiongozi wa warsha, hata hivyo, hii inaonesha kipimo cha uelwa wa washiriki kuhusu, na ni wakati gani kuna ufahamu wa ndani. Kiongozi wa warsha anaweza kulinganisha maandiko ya washiriki na ukweli na, ikiwa ni lazima, kuongeza na kufanyia kazi yaliyomo ambayo yatachukuliwa na washiriki katika vikao vya baadaye vya warsha.

**Tofauti:**

Njia iliyoelezwa haipaswi kutegemea picha, video au filamu pia zinaweza kutumika kama msingi, ambapo washiriki huchora mwigizaji na kuandika maandishi ya mimi…. kwa mtazamo wake. Aidha, maelezo ya mimi-….. hayapaswi kuandikwa mmoja mmoja; zinaweza pia kutumika kwa mpenzi au kazi ya kikundi ambapo washiriki wanajadili hali hiyo na kulinganisha hisia zao na kila mmoja na kuandika maandishi ya pamoja juu yake. Hasa katika tafakari, hii inaweza kuwa jambo muhimu wakati makundi yanapozungumzia tafsiri zao tofauti na juu ya hoja zipi wamekubaliana.

Tofauti bila matumizi ya vyombo vya kuandikia.

Kama njia mbadala ya kuandika maandiko ya mimi…, washiriki wanaweza pia kufikiria monologia na kuzielezea kwa mdomo. Washiriki wanapaswa kwanza kujibu maswali yaliyoelezwa na kisha wanaweza kuelezea kwa jumla jinsi watakavyojibu maswali kuhusu mtu aliye kwenye picha.

**Vifaa:**





**Njia ya 5: : Kikaragosi**

Kukuza uelewa katika kushughulika vyombo vya habari na habari; kutambua sifa za taarifa za uongo

Takribani miaka 12- 18.
Njia hii inahitaji washiriki kati 2-20. Namba Lazima iwe inagawanyika kwa 2

Kikaragosi (kinachoonekana kwa wote ama kwa vichapisho vyote au kilichoonyeshwa ukutani

Dakika 20-30 .

Mbinu inayolenga lugha: Inafaa kwa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika kwa sababu katuni zitatumika.

**Awamu za warsha: Mbinu hiyo inalenga SDG 14 (Bahari na rasilimali za baharini).**

**Utaratibu:**

Kiongozi wa semina anachagua kikaragosi kulingana na mada itakayoshughulikiwa, ambayo inachambuliwa katika mkutano. Ni vyema washiriki wote wakawa na mtazamo mzuri wa kikaragosi ili waweze kushiriki katika uchambuzi. Uchambuzi wa katuni hupitia awamu kadhaa:

1. Awamu ya maelezo na kuweka katika kundi kwa muda mfupi. Katika awamu hii, lengo ni kukielezea kikaragosi. Kiongozi wa semina anapaswa kuahirisha majaribio yoyote ya tafsiri ili kuepuka tafsiri ya haraka. Hii ni muhimu kwa sababu tafsiri ambayo hufanywa haraka mara nyingi inaweza kuwa na makosa zaidi.

2. Awamu ya ufafanuzi. Wakati wa awamu hii, uwezekano wa kwanza kuhusu mada unaweza kutajwa kwa namna ya katuni. Maudhui pia hujadiliwa kwa undani zaidi na maana ya alama na maudhui hutafsiriwa. Hairuhusiwi kueleza maoni binafsi katika hatua hii, kwani inahusu tu ujumbe wa katuni na hii haipaswi kutathminiwa.

3 Awamu ya tafsiri. Katika hatua hii, mtazamo wa mchora katuni unalinganishwa na mtazamo wa washiriki wenyewe. Washiriki hawapaswi kukubaliana na maoni ya mchora katuni, lakini maoni yao wenyewe yanapaswa kuthibitishwa kwa hoja.

Ili kupitia awamu hizi, maswali yafuatayo yanaweza kutumika kama mwongozo:

**Awamu ya maelezo na mpangilio:**

Naona nini kwenye picha/kikaragosi?

Je, kikaragosi hiki ni cha mwaka gani?

Ni watu/vitu gani vinavyooneshwa?

Vitu/watu vinaoneshwaje (k.mf. vikubwa sana au vidogo)?

Watu au vitu hivi vinafanya nini (action)?

Je nyuso zao zinatoa ishara na muonesho gani?

Je, kuna vipengele vyovyote vya kula njama?

**Awamu ya kutafsiri:**

Ni somo gani linaloibuliwa na kikaragosi?

Alama na vipengele tofauti ndani ya katuni vinamaanisha nini?

Ni akina nani walio ndani ya kikaragosi hiki (watu maarufu)?

Je, kuna uhusiano kati ya picha na maandishi? Ni upi?

Kiini cha katuni ni nini?

**Awamu ya ufafanuzi**

Kwa nini suala hili la kikaragosi linafaa?

Nini maoni ya mchora katuni? Nini maoni yako?

***Vyanzo vya makosa***

*Ili kuwasaidia washiriki, kiongozi wa semina anapaswa kufahamu vyanzo hivi vinavyowezekana vya makosa ikibidi waweze kukabiliana navyo. Mara nyingi makosa katika uchambuzi wa katuni hutokana na kufanya kazi haraka sana na kikijuujuu. Makosa ya mara kwa mara yameorodheshwa*:

- Maelezo yasiyo sahihi ya picha / vipengele vilivyooneshwa kutokana na ishara na muonekana wa uso havizingatiwi.
- Hii inaweza kusababisha tafsiri potofu ya kikaragosi.
- Kutozingatia awamu za mtu binafsi, tafsiri ya mapema sana au maelezo ya kuchelewa sana.
- Inaweza kusababisha tafsiri ya mapema sana ambayo haizingatii mambo muhimu.
- Kutoshika ujumbe mkuu wa katuni.
- Inawezekana kwamba maana iliyofichwa inayoakisiwa katika kikaragosi haieleweki, hii inaweza kuwa kwa sababu ya ukosefu wa taarifa

**Tafakari:**

Njia hii inaweza kutumika kujua jinsi gani washiriki walivyopenda njia ya kikaragosi. Aidha, kuwe na uwezekano wa washiriki kutoa mapendekezo ya mabadiliko. Hii inaweza kukusanywa na kiongozi wa semina na kuzingatiwa wakati ujao.

Maoni haya yanaweza kusaidia katika tathmini:

Ulifikiria nini kuhusu njia ya uchambuzi wa kikaragosi?

Je, ulikuwa na matatizo yoyote katika kutekeleza mbinu hiyo?

Je ni nini hasa kilikua rahisi?

Ni nini Ungebadilisha wakati ujao?

**Tofauti:**

Vinginevyo, uchambuzi wa filamu pia unaweza kufanywa kulingana na mpango huu. Ama eneo maalum ndani ya filamu linaweza kufikiwa, au filamu huwekwa katika mapumziko wakati fulani na picha iliyooneshwa inachambuliwa. Tofauti nyingine inayowezekana itakuwa kufanya uchambuzi wa katuni katika vikundi vidogo. Hizi zitakuwa na washiriki wa 2-4 kwa kila kikundi. Tofauti hii inatoa uwezekano kwa washiriki kati ya kikundi kupata nafasi ya kuelezea tafsiri yao mara nyingi zaidi. Kwa kuongezea, vikaragosi tofautitofauti vinaweza kutumika kwa kila kikundi na kuwasilishwa baadaye. Hata hivyo, tofauti hii inapaswa hutokea tu baada ya njia kurudiwa mara kadhaa, ili washiriki wajue ni nini muhimu katika uchambuzi wa katuni. Vinginevyo, washiriki wanaweza kuzidiwa na kazi.

Uwezekano mwingine utakuwa kuwaruhusu washiriki kubuni kikaragosi wao wenyewe katika hatua ya baadaye. Hii itahamasisha ubunifu wa washiriki na kuleta maoni yao wenyewe. Tofauti hii ingewezekana kwa mtu binafsi na kikundi.

**Vikaragosi:**

Vikaragosi ni aina ya kutoa maoni ambayo mara nyingi hukosoa mada au watu fulani. Kwa hivyo, wachoraji wa katuri huzidisha mada kwa makusudi ili kufanya ujumbe au pia ukosoaji wa mada kuwa wazi. Kutia chumvi zaidi kuna kunaongeza thamani ya burudani.

***Chanzo**: cf. O.A. (August 14, 2013). Bundeszentrale für politische Bildung. Karikaturen https://m.bpb.de/lernen/grafstat/grafstat-bundestagswahl-*

**Vifaa:**







*Newspaper*

*Umoja wa nchi za Ulaya: wazuia matumizi ya plastiki za matumizi ya maramoja*


©2019 The Toledo Blade
email: kirk@theblade.com
KIRK
Haikunusumbua matakataka ya plastiki kuzagaa baharini, mpaka nilipogundua kuwa sasa….,
…tunaweza kwenda Uingereza kwa miguu kutokea Ulaya


Gatis Sluka

**Njia ya 6: Maisha duniani**

**Maandalizi** Kutoa vifaa, kuunda mduara wa washiriki

**Maelezo:** Washiriki (TN) hujenga minyororo ya chakula na kujifunza mambo mbalimbali chanya au hasi yanayoathiri minyororo.

Kutegemeana kwa viumbe hai.
Kujifunza kushirikiana na kufikiria

Kuanzia umri wa miaka 14. Kiwango cha utata kinaelezwa kuwa cha kati. Ukubwa wa kikundi unapaswa kuwa kati ya watu 10-15.

Mpira wa uzi na kamba nyembamba

Dakika 30

Mbinu inayolenga uandishi: Inafaa kwa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika ikiwa kutakua na uwasilishaji picha zilizobandikwa pekee, badala ya vichwa vya habari.

**Awamu za warsha: Awamu ya utangulizi na ya kutambua matatizo**

**Utaratibu:**

Sehemu ya 1*: : Uundaji wa Mtandao wa Maisha*[44]



*1.* Washiriki wote (TN) wanajipanga katika duara.
2. Kiongozi wa warsha anaeleza kuwa minyororo ya chakula inatakiwa kuwakilishwa na kamba.

3. Kisha kiongozi wa semina anaanza mnyororo.

[44] Picture's source: https://www.wald.de/waldwissen/die-nahrungskette-im-wald/

Mwezeshaji huchukua mpira na kutaja mmea (k.mf. mti wa mikoko). Sasa anashikilia mwisho wa mpira na kuutupa kwa mshiriki mwingine upande wa pili. Hii inajenga kamba kati ya mwezeshaji na mshiriki.

4. Mshiriki sasa anamtaja mnyama anayekula mmea (k.mf. mjusi). Kisha wanashikilia kamba tena na kurusha mpira kwa mshiriki anayefuata.

5. Mshiriki kisha anamtaja mnyama anayekula aliyetangulia (k.mf. nyoka). Mshiriki anashikilia kamba na kurusha mpira kwa mshiriki mwingine.

6. Washiriki hurudia hili hadi mtandao wa maisha utakapoundwa. Ikiwa hakuna kiumbe kingine cha kuendeleza mnyororo huu, mpya unaweza kuanza. Jaribu kuhakikisha kuwa washiriki wanatumia makazi tofauti kwa minyororo (misitu, milima, moors, jangwa, mito, ...). Ikiwa ni lazima, elezea uhusiano kati ya sehemu binafsi za mnyororo wa chakula. Hata hivyo, kamba haiingiliwi wakati mnyororo mpya unaundwa lakini inaendelea. Mchezo unaendelea hadi kila mshiriki ashike sehemu ya kamba mkononi mwake.

*Sehemu ya 2: Uharibifu*

1. Washiriki sasa wanataja mifano mmoja baada ya mwingine ya vitu vinavyoweza kuharibu mpangilio huu. Kwa mfano, uvuvi wa kupita kiasi wa bahari, kusababisha jangwa, ukataji miti, n.k. Kila mshiriki ambaye ametoa mfano sasa anaachia sehemu yake ya kamba.

2. Washiriki huangalia rundo la kamba ambalo sasa liko mbele yao.

Sehemu ya 3: Kutafakari kuhusu utunzaji wa mazingira

1. Wanachama wote hufikiria kwa pamoja juu ya nini wanaweza kufanya ili kuboresha hali ya maisha kwa mimea, wanyama na watu. Kwa mfano, kutotupa takataka maeneo ya asili, kutochafua vyanzo vya maji na vitu vyenye madhara au kukuza viumbe hai katika bustani (shule). Kila mshiriki anachagua shughuli ambayo anataka kutekeleza katika maisha yake katika siku zijazo.

2. Kila mshiriki aliyechagua shughuli akuchukua sehemu yoyote ya kipande cha kamba.

3. Mwisho, washiriki wanaangalia wavu mpya kwa dakika moja. Eleza kuwa sio wavu sawa na mwanzoni. Matokeo ya uharibifu wa asili hauwezi kutatuliwa bila kufuatilia, lakini suluhisho mbadala na aina ya utulivu vinaweza kuanzishwa.

Anuwai ya kibiolojia, au bayoanuwai, hufafanua wanyama na mimea mbalimbali duniani wanaoishi pamoja katika makundi fulani katika maeneo fulani. Hizi ni muhimu zaidi kwa hali ya hewa na usambazaji wetu wa maji, lakini pia kwa ulinzi dhidi ya mafuriko. Uhifadhi wa bioanuwai kwa hiyo pia ni jambo muhimu katika kukomesha ongezeko la joto duniani.

***Chanzo****:cf.* *https://www.bmbf.de/bmbf/de/forschung/umwelt-und-*

**Tafakari:**

Anza kwa kuuliza jinsi washiriki walivyohisi walipoangalia kwa mara ya kwanza mtandao ukiharibiwa na kisha kuunda mpya. Kisha zungumzia masuala ambayo yamejitokeza na nini kifanyike ili kulinda mazingira. Aidha, jadili minyororo ya chakula na ueleze umuhimu wake (angalia sanduku la maelezo).

*Maswali kwa rejea:*

- *Ulijisikiaje kuona mtandao huo ukisambaratika taratibu?*
- *Je, ilikuwa rahisi kutaja wanyama na mimea katika sehemu tofauti katika mnyororo wa chakula?*
- *Je ni kwa kiasi gani tunajua vizuri kuhusu michakato katika asili (wanyama, mimea na mazingira)?*
- *Je, inajalisha kwa washiriki na mazingira yao ikiwa viumbe hai katika maeneo mengine ya dunia, kwa mfano dubu weupe katika Aktiki, wanatoweka katika miaka kumi ijayo? Hii ingekuwa na athari gani?*
- *Washiriki walijisikiaje wakati mtandao mpya ulipoundwa?*
- *Je, ilikuwa rahisi kuja na mawazo ya kupunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na binadamu?*
- *Vitendo vya mtu binafsi vina ufanisi kiasi gani? Ni vitendo gani vinavyohitaji ushiriki wa watu wengi, ni vipi vinaweza kuleta mabadiliko makubwa? Watu wanawezaje kufahamishwa na kuhamasishwa kuhusu hili?*
- *Nani anahusika na utunzaji wa mazingira?*
- *Ni vigezo gani vitumike kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya rasilimali na hatua katika mazingira ya asili? Kwa mfano, kama kukata msitu ili kutumia ardhi kwa kilimo?*

**Njia ya 7: Mtandao wa buibui**

Maandalizi: Ning'iniza "mtandao wa cbuibui" kati ya miti miwili au kitu kingine kama miti. Ikiwezekana, kuwe na idadi sawa ya matundu sawa na washiriki, wavu lazima unyooshwe kwa nguvu

Tambua, elewa na uweze kutumia nguvu na udhaifu wa wengine na wewe mwenyewe. Kuwa na uwezo wa kuwasiliana kwa uwazi juu ya nguvu na udhaifu

Kuanzia umri wa miaka 10. Ukubwa wa kikundi unapaswa kuwa kati ya watu 10-20.

Kamba ndefu (Urefu unategemea idadi ya washiriki)

Dakika 45-90

Mbinu inayolenga mchezo: inafaa kwa watu wasiojua kusoma na kuandika

**Awamu za warsha: Awamu ya utangulizi na ya kutatua matatizo**

**Utaratibu:**

**Maelezo** Kikundi kinapaswa kufikiria pamoja kuhusu washiriki wote wanaweza kufika upande wa pili wa wavuti wa buibui. Wanahitaji kufanya kazi pamoja, kuwasiliana kwa uwazi na kuona nguvu na udhaifu wa kila mtu fursa.

**1.** . Kundi linasimama pamoja upande mmoja wa wavu wa buibui. Mwezeshaji anatoa maelekezo yafuatayo:

a. Kila shimo kwenye wavuti linaweza kutembea mara moja tu.

b. Katika mazingira yoyote hautakiwi kugusa nyuzi za wavu, ukigusa utakua umeshindwa zoezi hilo linachukuliwa kupotea na wale wote ambao tayari wameshapita wavuni lazima warudi kwenye nafasi ya kuanzia. Kundi zima linarudia.

c. Ikiwa mshiriki mwingine pia anagusa wavu, kanuni hiyo hiyo inatumika kama hapo awali.

d. Usalama kwanza: epuka tahadhari na mbinu hatarishi na kuzikatiza ikibidi.

**2.** mwezeshaji anapaswa kuzingatia tu na kwa uwazi kusisitiza kuhusu uzingatiaji wa kanuni: Hata kama ni mshiriki mmoja ndiye aliyevunja kanuni, kila mtu anarudishwa.

Hii inaweza kusababisha kuchanganyikiwa na malalamiko, lakini yote ni mazuri kama zoezi hili litatoa matokeo mazuri

**3.** Kwanza kabisa, baadhi ya washiriki hupitia matundo rahisi kwenda upande wa pili. Kisha washiriki zaidi wanapaswa kubebwa kupitia matundu. Tena, lazima kusiwe na mawasiliano na wavu. Kikundi kinapaswa kukumbuka katika hatua ya awali kwamba hata washiriki wa mwisho lazima bado waweze kupanda kupitia wavu kwa kujitegemea..

**Tafakari:** Kiongozi wa semina anahimiza kikundi kujadili kwa kuuliza maswali yafuatayo:

- ✓ Je, mwanzoni mlikua na utata kukubaliana katika kundi kuhusu ni nani apite shimo gani la wavu wakati gani? Kama ndivyo, ulikabiliana vipi na hali hii?
- ✓ Kwa kuzingatia, unahisi kwamba nguvu na udhaifu wa kila mshiriki ulikusaidia kupata suluhisho?
- ✓ Unaweza kufikiria kwamba kuna watu ambao hawangepata msaada wa kutosha kuuvuka "wavu wa buibui"?
- ✓ Unaweza kufikiria mifano ambapo watu wasio na nguvu wanaachwa nyuma katika jamii?

**Tofauti:**

Mshiriki akigusa wavu, kiongozi wa semina humpa ulemavu (handicap). Mifano ya ulemavu inayowezekana: Kufumba macho au kuendelea kucheza bila maneno.

**Njia ya 8: : Kipindi cha mazungumzo (talkshow)**

Kuhimiza uwezo wa kujenga hoja,
Kuhimiza uwezo wa kujieleza, Kuhimiza majadiliano ya mada mbalimbali.
Mada Mambo Lengwa.

Kuanzia takribani Miaka 10-18. Kiwango cha utata kinakadiriwa kuwa kigumu.

Index card, karatasi, yaliyomo kwenye uwanja mmoja wa somo

Dakika 120.

Mbinu inayozingatia lugha: Inawafaa wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika.

Awamu za Warsha:

**Maandalizi::** : Uteuzi wa mada ya semina, na uteuzi wa taarifa, katika kikundi.

**Maelezo:** Washiriki wanachukua majukumu tofauti na kuzungumza mada kutoka kwenye jukumu lao.

**Utaratibu:**

Kipindi cha mazungumzo ni njia ambayo inafananishwa na uchezaji wa igizo. Mwanzoni, vikundi vidogo vinaundwa vikiwa na watu wawili hadi sita. Ndani ya kikundi hiki kidogo, mada, ambayo ilichaguliwa kabla au kutolewa na kiongozi wa semina, inafanyiwa kazi. Taarifa kuhusu mada hiyo inatolewa na kiongozi wa semina. Taarifa hizi zifanyiwa kazi ndani ya kundi dogo na kutuambua misimamo mbalimbali kutokana na maandishi. Majukumu ya kipindi cha mazungumzo hapo baadaye yanatokana na nafasi hizi tofauti. Mada ya kipindi cha mazungumzo inaweza kuwa endelevu, kwa mfano, rejea maalum zaidi inaweza kuwa kuchakata tena na marufuku ya mirija ya plastiki duniani kote. Misimamo tofauti inayotokana na hili inaweza kuwa, kwa mfano, kuwa na marufuku ya mirija ya plastiki au kuunga mkono mirija hiyo. Hii inaweza kusababisha majukumu tofauti. Kwa upande mmoja, jukumu la watumiaji/walaji ambao kwa hivyo hawaruhusiwi kutumia mirija ya plastiki, jukumu la wazalishaji waliozalisha mairija ya plastiki na jukumu la wataalamu wanaoelimisha watu duniani kote kuhusu matumizi ya plastiki na madhara yake. Kulingana na majukumu haya, washiriki wanaorodhesha hoja na kuziandika kwenye kadi ili waweze kuzileta kwenye kipindi cha mazungumzo baadaye. Nafasi na jukumu lingine ambalo lazima lijazwe na kuamuliwa mapema ni lile la msimamizi. Msimamizi lazima asiegemee upande wowote kwa wageni wake na hapaswi kutanguliza maoni binafsi. Uangalifu lazima uchukuliwe kuzingatia kanuni za majadiliano na kuhakikisha kuwa washiriki wote wanaweza kuwasilisha hoja zao. Aidha, maswali lazima yaulizwe ili kuendeleza mazungumzo/majadiliano. Hatimaye, msimamizi ana kazi kuchora hitimisho kutokana na maudhuui na kuyawasilisha kwa hadhira. Ndani ya njia hii, washiriki wote wanakabiliwa na changamoto sawa, kwani washiriki ambao sio wa kikundi kinachowasilisha kwa sasa wanachukuliwa kama watazamaji wa kipindi cha mazungumzo na wana zoezi la kuchunguza kinachotokea (ikiwa wanataka, wanaweza pia kuuliza maswali).

**Njia ya 9: Muhtasari wa majukumu**

***Kuongoza:*** *Zoezi la kuongoza majadiliano na kutoa msukumo. Kuhakikisha kuwa sheria za mazungumzo zinazingatiwa. Fungua kipindi cha mazungumzo kwa kuwakaribisha na kuwatambulisha wageni na kumaliza kipindi cha mazungumzo kwa hitimisho*

***Wageni*** *Waalikwa: Majukumu mbalimbali yanayochukuliwa na washiriki. Toa maoni juu ya mada na uwe na msimamo wa wazi katika mjadala.*

***Bunge:*** *Hawa ni washiriki ambao si sehemu ya kundi. Wana zoezi la kuchunguza kipindi cha mazungumzo na wanaweza kuuliza maswali ikiwa wanataka.*

**Utaratibu:**

**1.** 1. Kukaribisha na kutambulisha wageni na mada (itachukuliwa na msimamizi, wageni wanaweza, kutoa maoni kuhusu mada)

2. Majadiliano na wageni mbalimbali (wakiongozwa na msimamizi, kuhakikisha kuwa sheria za majadiliano zinazingatiwa)

3. Maoni ya hitimisho kutoka kwa wageni (ufahamu au maoni yanaweza kutolewa tena na kila mgeni)

4. Hitimisho (litafanywa na msimamizi)..

**Tafakari:**

Rejea kuhusu njia inafanyika kwa ujumla na kwa mdomo. Inajadiliwa pamoja na washiriki wote kuhusu majukumu ya washiriki binafsi na misimamo yao katika majadiliano. Kwa hiyo, hoja ambayo ililetwa katika kipindi cha mazungumzo inajadiliwa tena kwa undani. Uwezekano mwingine ni kuwapa mrejesho wanakikundi kama walikuwa na ushawishi katika misimamo yao. Hata hivyo, hii inahusu hoja tu na si kukubaliana au kutokubaliana na hoja. Maoni haya yanaweza kusaidia katika majadiliano ya baadaye kuunda hoja kwa usahihi na kuzianzisha katika maeneo yanayofaa.

**Tofauti:**

***Tofauti za kujihariria taarifa:***

Washiriki pia wanaweza kufanyia kazi taarifa ambazo zinafaa kwa kipindi cha mazungumzo. Hii inawahimiza kujihusisha na mada na pia inawasaidia katika kukusanya habari kwa mijadala ya baadaye. Ikumbukwe kuwa utafiti wa kujitegema

utachukua muda zaidi na hivyo somo la ziada llipangiwe muda mtefu (mara mbili ya kawaida) kwa swala hili pekee. Uwezekano mwingine ni kwamba washiriki huandika kipindi cha mazungumzo kabla, kama maandishi ya tamthlia wawe na ujasiri zaidi na waweze kuzisoma ikiwalazimu. Hata hivyo lile wazo yakinifu la kuandaa hoja kwa wakati sahihi na kuwasilisha ni kama linapotea hivi.

***Tofauti bila matumizi ya vyombo vya kuandikia:***

Uwezekano mwingine ni kutoandika kwenye kadi za faharisi. Kwanza, mada tofauti zinaweza kufanyiwa kazi kwa jumla na washiriki huchagua msimamo wao. Baadaye, wanakaa chini mbele katika duru ya kipindi cha mazugumzo na kuwa na mjadala huru. Hata hivyo, hii ni ngumu zaidi na inaweza kuhitaji msaada wa ziada kutoka kwa kiongozi wa warsha.

**Njia ya 10: Mjadala wa kuunga na kupinga hoja**

Kuhimiza kuunda na kuwakilisha maoni ya mtu mwenyewe,
Hoja na usemi wa lugha

Kuanzia takribani miaka 14-18.
Sharti ni idadi sawa ya washiriki.
Kiwango cha utata kinakadiriwa kuwa kigumu.

Hakuna nyenzo zinazohitajika.

Kuanzia mmoja na zaidi

Mbinu inayolenga lugha: inafaa kwa wanawake wasiojua kusoma na kuandika. Badala ya majina, ishara au sawa inaweza kutolewa ili kutambua kadi.

**Awamu za warsha:**

**Maandalizi:** Mgawanyiko katika timu, uchaguzi wa msimamizi, kukiwa na haja ujuzi wa msingi wa uwanda wa mada unahitajika.

**Maelezo:**

Wanagawanywa katika jukumu la kuunga mkono au kupinga juu ya mada na hoja kutoka kwa jukumu hili.

Tofauti kati ya hii na kipindi cha mazungumzo ni kwamba majadiliano rahisi, wakati kipindi cha mazungumzo kinaweza tu kuwa na habari na kufundisha.

**Utaratibu:**

Hoja kuu ya njia hii ni kuunda hoja na kuzielezea. Mwanzoni, mada ya mjadala inaelezwa na kiongozi wa semina. Hii inaweza kuwa hoja au swali. Kwa mfano: "Ushirikiano wa nchi zote kwenye malengo ya ESD ni muhimu!" Au pia "Kwa nini nchi nyingi zishiriki katika malengo ya ESD?". Yote haya yanaruhusu mjadala wa kuunga au kupinga hoja. Washiriki ambao wanaona ushirikiano kati ya nchi kuwa muhimu (pro) na wale ambao hawaoni (contra). Hakikisha kuwa pande zinazounga mkono na zisizounga mkona zina usawa, na sio washiriki wa 5 wanapinga upande wa mkataba na 12 wanaunga mkono. Kiongozi wa semina lazima ahakikishe kuwa kuna usawa. Aidha, msimamizi huchaguliwa; Jukumu hili linaweza kuchukuliwa na kiongozi wa semina au na mmoja wa washiriki. Zoezi la msimamizi ni kuhakikisha kwamba kanuni za majadiliano zinazingatiwa, kwamba hoja zinaweza kutekelezwa kwa busara bila mgogoro kujitokeza, bali mjadala unabaki kuwa lengo. Msimamizi pia anaweza kuchukua jukumu la kusaidia, kwa mfano kwa kuuliza maswali. Baada ya makundi mawili tofauti kupatikana, msimamizi anafungua mjadala. Msimamizi anaelezea swali au hoja tena, na washiriki tofauti sasa wanaweza kujibu. Jambo muhimu zaidi hapa ni kwamba hoja pia zinarejelewa na kwamba ukweli na madai hayawekwi tu chumbani. Ikiwa mtu A anasema kuwa ushirikiano unawezesha kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, mtu B anapaswa kujaribu kurekebisha kauli hii na sio tu kutoa taarifa mpya ya kujitegemea. Msimamizi lazima pia ahakikishe kuwa washiriki hawakai muda mrefu kwenye hoja moja, ili ukweli mwingine na madai pia yaweze kujadiliwa. Kulingana na kama washiriki wote wameshiriki katika shughuli hiyo au wengine wamefanya kama watazamaji, umma unaweza kuchagua kikundi kilichoshinda. Hata hivyo, hii inapaswa kuzingatia uwezo wa kikundi kujenga hoja na sio kwa mtazamo wao binafsi juu ya mada

**Maswali/hoja zinaweza kuwa:**

- ✓ Hasa nchi zilizo bora kiuchumi lazima zishirikiane kuzisaidia nchi maskini.
- ✓ Je, nchi "maskini" zitengwe katika ushirikiano huu?
- ✓ Nchi zote lazima zishirikiane katika viwango sawa, bila kujali wingi wa rasilimali zao.
- ✓ Maoni tofauti ya nchi yanamaanisha kuwa hakutakuwa na makubaliano, kwa sababu hii nchi zinapaswa kutenda kivyakevyake.
- ✓ Nchi ndogo hazipaswi kuzingatia hatua za uhifadhi wa na hali ya hewa hadi nchi kubwa zifanye hivyo; kitu kingine chochote hakitakuwa na athari yoyote.
- ✓ Je, uhifathi mazingira na hali ya hewa unaleta maana ikiwa Urusi, China na Marekani hazitashirikiana?

Rejea:

- ✓ Hizi ni baadhi ya rejea zinazoweza kutafakariwa ambazo zitasaidia kutathmini njia hii
- ✓ Uliridhika vipi na msimamo wako (kuunga mkono au kupinga)?
- ✓ Ilikuwa rahisi au ngumu kiasi gani kwako kupata na kutengeneza hoja za swali/hoja hii?
- ✓ Je, ungeuliza swali/hoja vinginevyo wakati mwingine?
- ✓ Uliona nini hasa rahisi au ngumu kuhusu njia hii?
- ✓ Utabadilisha nini kuhusu njia wakati mwingine?

**Tofauti**:

Inaweza pia kuchezwa na kundi zima bila kusanyiko. Zaidi ya hayo, jozi tu zinaweza kufanya mijadala, kwa uwiano wa mshiriki mmoja dhidi ya mwingine. Hata hivyo, mijadala hii inapaswa kuwekwa kwa muda mfupi zaidi.




https://blog.codecentric.de/2018/11/konflikte-in-teams-loesen/

**Ujuzi wa msingi wa usimamizi wa migogoro**

Tafsiri ya mgogoro:

Migogoro ni mchakato wa mabishano kulingana na masilahi na mawazo ya mtu ambaye ni sehemu ya kikundi cha kijamii. Inapaswa kusisitizwa, hata hivyo, si lazima migogoro iwe mbaya kila wakati.

Kwa sababu dhana ya migogoro ni pana, aina tofauti za migogoro pia huibuka. Ikiwa pande zote mbili zinafahamu mgogoro huo, aina hii ya migogoro huitwa mgogoro wa wazi. Ikiwa ni wazi kwamba mgogoro unaweza kutokea kutokana na hali hiyo, lakini bado hakuna mgogoro, mgogoro huu unaitwa mgogoro tuli (latent).

Kama watendaji wote wawili wanategemeana, lakini wanafuata malengo tofauti, huu ni mgongano wa malengo. Kwa upande wa mgogoro wa tathmini, mbinu zinazotumika kupata lengo hutathminiwa tofauti. Kunapokuwa na maamuzi tofauti ya kisaikolojia na ya kitabia, huu ni mgogoro binafsi. Wakati kutofautiana hutokea katika uhusiano kati ya watu, huitwa mgogoro wa uhusiano. Mgogoro wa kimahusiano hujitokeza pale watu wanapotekeleza majukumu tofauti na hivyo kuwekwa wazi katika matarajio ya jukumu hili.

(https://wirtschaftslexikon.gabler.de/definition/konflikt-41120 )




*Je ungependa kuwa sahihi au kuwa na furaha?*

**Ufafanuzi wa usimamizi wa migogoro**

Udhibiti wa migogoro unahusisha utambuzi, usimamizi na udhibiti wa migogoro kupitia aina tofauti za kushughulikia kama vile mazungumzo, upatanishi, maridhiano na usuluhishi wa lazima.

https://wirtschaftslexikon.gabler.de/definition/konfliktmanagement-41409

**Mgogoro unaibuka vipi?**

Migogoro daima huanza na ukinzani wa mawasiliano unaofuata mawasiliano ya awali. Katika mahusiano ya kijamii, migogoro hii kwa kawaida husababishwa na matarajio yasiyotimia ya upande mwingine au kutofikia muafaka wa mambo ambayo hawajakubaliana. Migogoro daima huanza wakati wa maingiliano ya watu. Haijalishi kama mawasiliano yanayotokana yana maneno au muonekano wa sura na ishara. (Thiel, 2003)

**Usimamizi wa migogoro ni nini?**

**Migogoro inawezaje kutatuliwa na kuzuiwa?**



https://www.in-stability.de/de/entwicklungsberatung/leistungen/konfliktmanagement-und-meditation/

Njia mojawapo ya kutatua migogoro ni kuingilia kati, ambayo inatafuta suluhisho la kutatua mgogoro. Njia nyingine yenye ufanisi mkubwa ni kuleta mtu wa tatu, asiyehusika. Mtu huyu anapaswa kuchunguza mgogoro kwa njia isiyo na upendeleo na kusaidia kupata suluhisho. Ushiriki huu wa mtu wa tatu kutatua migogoro pia unaweza kuitwa de-escalation (kuzuia kasi kuenea kwa mgogoro) , kama ufafanuzi wa kuondoa migogoro unavyosema kwamba inamaanisha kupoozesha mifumo ya migogoro. Ili kupunguza kasi ya kuenea migogoro, athari za pamoja lazima zipunguzwe. Kwa kufanya hivyo, haitoshi kushusha hali ya kihisia mpaka kiwango kilichokuwa kabla ya mgogoro kuanza na kabla ya kuongezeka. Badala yake, ni muhimu kuhakikisha kuwa hisia zinakuwa thabiti zaidi na kuna utulivu zaidi katika hali ya kihisia kuliko ilivyokuwa kabla ya mzozo. Kuna njia tatu ambazo kuzuia kasi ya kuenea kwa mgogogoro kunaweza kutokea. Namna ya kwanza hutokea baada ya kujitafakari, ambayo hutokea kwenye matukio ndani na nje ya mazingira ya mtu binafsi. Namna ya pili hutokea baada ya ushawishi na udhibiti wa muktadha wa mtu mwingine. Namna ya mwisho inafuatia uharibifu wa mfumo wa migogoro. Uingiliaji kati huu wa kuzuia kuenea kwa mgogoro ni muhimu zaidi unapotumiwa kuwafanya wahusika wakuu katika mgogoro kujua tabia zao.

Njia nyingine ya kutatua ni kuzuia migogoro. Hii inahusisha kuhakikisha kuwa migogoro haitokei tangia mwanzo. Hili linafanikiwa, pamoja na mambo mengine, kwa kutafuta mara kwa mara uwezo wa migogoro na kuitatua kabla ya kuja kwa migogoro. Uingiliaji kati wa Uponyaji (curative) pia unaweza kutumika kutatua migogoro. Uingiliaji kati wa uponyaji huingilia kati tu wakati mzozo tayari umeibuka. Inatathminiwa ndani ya uchunguzi ni dondoo zipi za mgogoro tayari zimeibuka na ni madai na matakwa gani tayari yametolewa na upande mwingine wa mgogoro. Kwa njia hii, njia ya suluhisho inaweza kupatikana ili kutatua mgogoro kulingana na maslahi ya pande zote mbili.

Njia nyingine ni kuongeza mzozo/mgogoro. Inachukuliwa kuwa njia ya kutatua migogoro kwa kuuongeza mgogoro. Katika njia hii, hatua za makusudi zinachukuliwa ambazo awali zinazidisha mgogoro, lakini zinaweza kusababisha kumalizika kwa mgogoro baada muda mrefu. (Meyer, 2011)

### Ukatili/Vurugu

**Ufafanuzi wa vurugu**

Ukatili hauanzii kwa kutumia nguvu za kimwili. Pia inajumuisha vitendo kama vile vitisho, unyanyasaji, na udhibiti uliowekwa wa mtu mwingine. Vurugu huathiri watu wa rika zote na tabaka zote za kijamii.

https://wirtschaftslexikon.gabler.de/definition/gewalt-33514



https://selam.berlin/gewalt-im-kontext-schule/

### Aina za vurugu

Ili kufafanua ni vitendo gani vimo ndani ya dhana ya kawaida ya vurugu, kwanza ni muhimu kufafanua ni aina gani za vurugu zilizopo.

Moja ya aina zinazojulikana zaidi za ukatili ni **ukatili wa kimwili**. Hii ni pamoja na mashambulizi yote dhidi ya mwili na afya ya mtu. Ukatili wa kimwili unajumuisha kila kitu kuanzia kumsukuma mtu kidogo hadi shambulio kwa silaha. Tofauti hufanywa kati ya mashambulizi butu na mashambulizi yenye ncha kali. Mfano wa mashambulizi butu ni kama kupiga ngumi, shambulizi la ncha kali linaweza kuwa kuchoma kisu. Tofauti pia hufanywa kati ya majeraha yanayoonekana na yasiyoonekana. Ukatili wa kimwili mara nyingi hutokea katika ndoa, ushirikiano na familia, kati ya watoto na vijana, miongoni mwa wageni, katika nyumba za wazee na nyumba za uuguzi, dhidi ya polisi, wazima moto na wafanyakazi wa uokoaji na dhidi ya wafanyakazi katika ofisi na mamlaka.

Aina nyingine ya ukatili ni **ukatili wa kisaikolojia**. Tofauti na ukatili wa kimwili, ukatili wa kisaikolojia au kiakili madhara yake hayaonekani. Ukatili wa kisaikolojia ni pamoja na vitendo kama vile kutukana, kukejeli na kufichua, dhihaka, hadi kutishia na kusingizia. Aidha, uonevu na uviziaji pia ni wa ukatili wa kisaikolojia. Moja ya matokeo mabaya zaidi ya unyanyasaji wa kisaikolojia ni kwamba hauonekani lakini unaweza kuhisiwa. Kwa hiyo inaweza kujeruhi vibaya watu na kuwa na madhara ya kiafya. Silaha iliyotumika ni neno linalotamkwa..

**Ukatili wa kijinsia** pia ni muhimu. Hii ni pamoja na vitendo vyote vya ngono vinavyotokea kinyume na matakwa ya mtu au vinavyofanywa kwa watu wenye umri wa miaka 14 au chini, bila kujali kama wanakubali tendo hilo. Hivi ni vitendo vinavyofanywa kwa wale ambao hawako katika nafasi ya kukataa. Ukatili wa kijinsia huanza na lugha zisizofaa na mgoso usiokubalika na mbaya zaidi huishia katika ubakaji. Ikumbukwe pia kuwa ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na vijana mara nyingi hutokea katika mazingira yao ya karibu. Kwa kawaida huwa wanamuona mtu huyo na wakati mwingine hata kufahamiana naye.

**Ukatili wa majumbani** majumbani daima hutokea kati ya watu walioolewa/kushirikiana au katika mahusiano, ni wa familia au kuishi pamoja, wametengana/kutalikiana. Lengo mara nyingi ni kutumia nguvu na kupata udhibiti juu ya mwenza. Ni muhimu kutambua kuwa unyanyasaji wa nyumbani sio kitu kinachotokea kwa bahati mara moja, bali ni mfululizo wa vitendo vinavyofuatana. Unyanyasaji wa nyumbani kwa kawaida hujumuisha aina nyingine zote zilizoorodheshwa za ukatili.

Aina mpya ya ukatili ni **ukatili wa kidijitali**. Kila mahali unaweza kuona mtandaoni, ukatili hutokea kila siku. Ukatili wa kidijitali unajumuisha vitu kama vile unyanyasaji wa

kimtandao, uonezi wa kimtandao, maoni ya chuki na unyanyasaji wa kijinsia. Jambo linalozidi kuongezeka katika ukatili wa kimtandao ni ukatili wa kijinsia unaofanywa na watu wazima na vijana na watoto. Wanajaribu kuwarubuni kwa picha na ahadi na bila aibu kutumia imani nzuri ya vijana.
Aina nyingine ya ukatili ambayo ni muhimu kutaja ni **ndoa za kulazimishwa**. Daima ni ndoa ya kulazimishwa ikiwa angalau mmoja kati ya hao wawili hakubaliani na ndoa hiyo. Mara nyingi, vitisho hutolewa ili kupitisha ndoa au wahusika hutishwa sana kiasi kwamba hawawezi kupinga familia zao na wala hawathubutu hata kujieleza kwamba wanapinga hilo. Ingawa visa zaidi na zaidi vya ndoa za kulazimishwa vinajitokeza, idadi ya visa ambavyo havijaripotiwa inakadiriwa kuwa kubwa zaidi.

**Njia ya 11: Kuingilia kati na mbinu dhidi ya ukatili**

Katika kutafuta suluhisho la tabia ya ukatili, semina ya utulivu na kupinga ukatili inaonekana kuwa na mafanikio makubwa kwa vijana wazima. Ni wazi zinafaa zaidi kuleta mabadiliko ya tabia kwa wahalifu wenye sifa mbaya na vijana wakali kuliko mbinu nyingine. Kwa vyovyote vile, dhana mojamoja hufanyiwa kazi, ambayo inapaswa kuwasaidia vijana kuitumia kama rejea na kuchukua hatua sahihi iwapo hali kama hiyo ikiwatokea siku zijazo na hivyo kutenda kwa usahihi. Kwa msaada wa mbinu hizi, huruma inapaswa kuendelezwa, hasa kwa waathirika, na pia kuna tafakari ya kina juu ya matendo ya mtu mwenyewe. Hatua kama hiyo pia inathibitisha kuwa ni bora zaidi kuliko kifungo bila tiba ya kisaikolojia, kwani wahalifu hawa mara nyingi hawajui kiwango cha matendo yao bila msaada wa matibabu na hurudia haraka sana mara tu wanapowekwa huru.
(https://www.researchgate.net/profile/Albert-Scherr/publication/242675979_Mit_Harte_gegen_Gewalt_Kritische_Anmerkungen_zum_Anti-Aggressivitats-_und_Coolness_Training/links/0a85e537b356e14a3f000000/Mit-Haerte-gegen-Gewalt-Kritische-Anmerkungen-zum-Anti-Aggressivitaets-und-Coolness-Training.pdf)

Njia nyingine ya kutatua vurugu ni kupitia taasisi zinazoshughulikia suala hilo.
Kuna mashirika ya msaada ambayo yamejikita kusaidia vijana ambao wanahitaji msaada katika hali mbalimbali. Wakati wowote msaada unapohitajika, unaweza kuwasiliana na taasisi hizi na watajaribu kukusaidia ili kuzuia vijana kupata msaada

mahali pasipostahili au kutelezea katika shughuli haramu. Muhimu zaidi ndani ya mada hii ni dhana ya kufanya ukatili kuwa suala kubwa.

Wameanzisha dhana ambayo hasa inalenga watoto wa shule za msingi, na wanapaswa kuhakikisha kuwa watoto hawa hawakutani na ukatili katika ujana wao. Sababu nyingine ya kuwalenga watoto wa shule za msingi ni kwa sababu elimu hii ni ya lazima hivyo inawezesha kufikia idadi kubwa ya watu.

Semina inayofanyika ndani ya dhana inaweza kugawanywa katika awamu sita:

1. **Maandalizi**
   - ✓ Mkufunzi anayeendesha semina anawasilisha kwa uwazi na mapema ni nini malengo mwishoni mwa vikao.
   - ✓ **Kuanzisha mawasiliano na mwelekeo,** Ni muhimu kama mtaalamu wa kigeni kufanya taswira nzuri wakati wa kukutana na watoto ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki
2. **Kuhamasisha**
   - ✓ Wanafunzi wanafahamishwa kuhusu suala hilo na kuelimishwa kwa vithibitisho na takwimu.
3. **Mikakati ya kitabia endapo kutatokea ukiukwaji wa mipaka na ukatili**
   - ✓ Watoto wanahusika kwa makusudi katika hali hii ya mazoezi ili waweze kujifunza mbinu za kuchukua hatua kwa siku zijazo.
4. **Kufunga na kuondoka**
   - ✓ Awamu hii haichukui muda mwingi na wanafunzi wanakumbushwa tu kuwa kikao cha masomo sasa kimekwisha.
5. **Uhamisho wa kila siku, ufuatiliaji na ufanisi**
   - ✓ Ni muhimu walimu na wazazi waendelee kutoa misukumo baada ya semina ili kuyaweka hai yale waliyojifunza. Vinginevyo, semina haitakuwa na athari ya muda mrefu. Ikumbukwe, hata hivyo, kwamba semina halisi hufanyika katika awamu ya 2 - 5.

(https://wellenbrecher.de/?gclid=CjwKCAiAvaGRBhBlEiwAiYyMIWAB1ji2x6lQkndkn2le85laTu0jQBjd98R7xYSnxkG4byDmLMlyhoCgz4QAvD_BwE ) )

**Mawasiliano**



[https://pixabay.com](https://pixabay.com)

**Ufafanuzi wa mawasiliano:**

Mawasiliano ni njia ya kubadilishana kati ya watu ambayo kwayo habari hupitishwa kati ya mtumaji na mpokeaji mmoja au zaidi. Hii inaweza kufanywa kwa njia tofauti. Inaweza kugawanywa katika mawasiliano yasiyo ya maneno na ya maneno. Mawasiliano ya maneno hufanyika kupitia usemi na mawasiliano yasiyo ya maneno hupitia lugha ya mwili kama vile sura za uso na ishara.




[https://pixabay.com](https://pixabay.com)

Mawasiliano yanafanyaje kazi?

Mwanasayansi wa mawasiliano wa Ujerumani Friedemann Schulz von Thun aliunda mtindo wa mawasiliano, pia unaitwa "four ears model", ambao unalenga kufafanua jinsi mawasiliano yanavyofanya kazi. Katika mtindo huu, kuna **mtumaji** na **mpokeaji**. Kila kauli ya mtu hubeba jumbe nne tofauti kwa wakati mmoja. Ujumbe huu pia humfikia mpokeaji kwa viwango vinne, kile kinachoitwa "masikio manne". Mtindo huu unawakilishwa katika mraba, ambao unaonyesha viwango vinne vya mawasiliano. **Ngazi ya kwanza ya maudhui ya ukweli** inahusika na ukweli na hali. Ngazi ya **kujitangaza** daima hushikilia kitu cha kibinafsi kama vile hisia, maadili, mahitaji au upekee wa aina fulani ya tabia. Haya yanaweza kuwa mawasiliano ya wazi na ukamilifu. **Kiwango cha uhusiano** kinaonyesha jinsi unavyohisi kuhusu mtu mwingine

na kile unachofikiria juu yake. Dalili hizi zinaweza kujielezea kwa msaada wa muonekano wa sura, ishara, sauti na maneno. Katika ngazi ya rufaa, matakwa, ushauri, maelekezo ya hatua au rufaa huwasilishwa. (von Thun et al., 2012)

**Nini maana ya mawasiliano yasiyo ya vurugu?**

Dhana ya mawasiliano yasiyo ya vurugu mara nyingi haieleweki vizuri. Mara nyingi huchanganywa na maelewano na mawasiliano bila migogoro na migogoro yoyote kabisa. Hata hivyo, hii sio maana ya mawasiliano yasiyo ya vurugu. Badala yake ni kushughulikia kikamilifu migogoro badala ya kuikandamiza kabisa. Ufumbuzi unapaswa kupatikana unaoridhisha pande zote mbili. Migogoro ya maslahi pamoja na tofauti za maoni ni kitu cha kawaida kabisa na ni sehemu ya maisha ya kila siku na ni muhimu sana kwa maendeleo yetu. Kwa hiyo, ni muhimu kutenda kwa usahihi katika hali hizi za migogoro, kutenda kwa huruma/uelewa, kuonyesha unajali binadamu wenzako. Daima kuna angalau pande mbili kwenye mgogoro. Makundi mawiwili yenye mtazamo, hisia na mahitaji tofauti. Inaweza kusaidia kubadili mtazamo wa mtu na kujaribu kuvaa viatu vya mtu mwingine. Kwa kutafuta ufumbuzi ambao una maslahi kwa pande zote za mgogoro (win win situation), mawasiliano yasiyo ya vurugu yanaweza kuwezeshwa. Ili kupata suluhisho hili, ushirikiano wa pande zote mbili unahitajika. Ushirikiano na mtazamo wazi juu ya mpatanishi/mwakilishi wa mtu na hisia na mahitaji yake. Ili kupitisha mtazamo huo wa wazi, njia ya mawasiliano yasiyo ya vurugu na Marshall B. Rosenberg inaweza kutumika.

Kwa hiyo, mawasiliano yasiyo ya vurugu hayamaanishi "Sisi daima ni wazuri kwa kila mmoja", "Hatutapaza sauti tena" au "Ninafanikiwa kwa matendo yangu kwamba kila mtu anafanya kile ninachotaka". Badala yake, ni kukabiliana na mgogoro pamoja na kila mtu kuonesha anajali ili pande zote mbili ziweze kuacha mgogoro zikiwa zimeridhika iwe sana au kidogo. (Basu & Faust, 2015)

**Mtu anachukuliaje mawasiliano yasiyo ya vurugu?**

Mawasiliano yasiyo ya vurugu ya Rosenberg humsaidia mtu kuunda mahitaji/matakwa ya mtu mwenyewe kwa njia ambayo mtu mwingine ananielewa, migogoro inaweza kuepukwa na kutatuliwa, mazungumzo yanaweza kufanyika kwa kiwango cha ana kwa ana na hali zinazomsumbua mtu zinaweza kushughulikiwa. Tofali muhimu zaidi katika ujenzi wa njia hii ni huruma/kujaribu kumuelewa mwenzako (empathy)



**Ufafanuzi huruma/Uelewa. Kujaribu kuvaa viatu vyao):**
Huruma/kuelewa wanzako huelezea uwezo na utayari wa kutambua na kuelewa hisia na mawazo ya watu wengine. Uelewa ni muhimu sana katika hatua za kutenda kimaadili.

(Rosenberg, 2016)

**Marshall B. Rosenberg - Mawasiliano yasiyo ya vurugu**

Mwanasaikolojia wa Marekani Marshall Bertram Rosenberg alitengeneza dhana ya mawasiliano yasiyo ya vurugu (GfK) ili kufanya mawasiliano yafanikiwe. Anatofautisha kati ya aina mbili za mawasiliano: wewe- na mimi-. Rosenberg anaelewa wewe- kama majaribio ya mawasiliano ambayo yana hukumu za maadili au tathmini, pamoja na ujumla, tafsiri, lawama na mahitaji. Kwa mawasiliano yenye tija, ni muhimu sana kuepuka vizuizi vya mawasiliano kwa kuacha kutumia jumbe za wewe. Ujumbe wako unaweza kuwa, kwa mfano, hukumu za maadili au tathmini kama vile "Huaminiki" au ujumuishaji kama vile "Tena? Kamwe wewe huwezi kuifanya kwa wakati.". Madai kama vile "Ikiwa hutabadilisha tabia yako, kutakuwa na madhara!" yanaweza pia kuweka shinikizo kwa mpokeaji na kuwa na kuondoa tija katika mawasiliano. Kwa jumbe za "wewe", vizuizi vya mawasiliano vinaweza kutokea ambavyo vinafanya iwe vigumu kutatua mgogoro.
Ujumbe wa “mimi”, kwa upande mwingine, unahusu kuelewa na kueleweka. Ili kufanya hivyo, lazima uwe na uwezo wa kuelezea hisia na mahitaji yako na kumsikiliza kwa huruma/uelewa mpatanishi/mwakilishi . Lengo ni kuepuka vikwazo vya mawasiliano, kuelewa na kueleweka. (Rosenberg, 2016)

**Njia ya 12: Mfano wa hatua nne**

Rosenberg ameunda **mfano wa hatua nne** ambao mawasiliano yasiyo ya vurugu yanatakiwa kufanikiwa.

**Hatua ya 1: Uchunguzi**




Kwanza kabisa, hali lazima izingatiwe. Hii inajumuisha kutambua mazingira na mtu mwingine na kurekodi kile kinachotokea katika hali hiyo. Ni muhimu kuzingatia kile mtu mwingine anasema na jinsi anavyotenda (muonekano wa sura, ishara, sauti).

Ni muhimu hasa hapa kuwasilisha kila kitu kwa mtu mwingine kwa njia isiyoegemea upande wowote kabisa bila tathmini na hukumu. Unaelezea kitu kinachofanywa na kama unakipenda au la. Kufuatia hatua hii kwanza hujenga msingi wa kawaida wa mazungumzo.

Ujumlishaji kama vile "daima, kamwe, tena, nk." unapaswa kuepukwa.

**Hatua ya 2: Hisia**

Hatua ya pili ni kuhusu kufichua hisia za mtu mwenyewe kuhusiana na hali. Hii ni muhimu ili mwenzangu aweze kunielewa vizuri na kuelewa matendo na maneno yangu ipasavyo. Kuelezea hisia zangu kunaweza kuwa na athari ya kupunguza mgogoro. Hapa, pia, ni muhimu kutenganisha hisia zangu na mawazo ya kusikitisha. Inaweza kutokea kwa urahisi kwamba mawazo yanatafsiriwa kama hisia na kuna hatari mzungumzaji wa upande wa pili ataona hili kama shambulio.

Hapa kuna mfano mdogo wa kuonyesha hii:

Badala ya kusema "Sihisi kwamba unanichukulia kwa uzito", unapaswa kuzingatia tu hisia zako mwenyewe na kujaribu kuzielezea kama "Ninahisi wasiwasi na kukereka

**Hatua ya 3: Mahitaji**

Katika hatua ya tatu, ni muhimu kutambua mahitaji ya mtu na kuyafichua kwa mzungumzaji wa upande wa pli. Ufichuzi huu wa mahitaji ya mtu hutoa fursa ya kueleweka vyema katika hali za migogoro. Orodha ya mahitaji ya binadamu inaweza

kupatikana katika kiambatanisho. Hii inaweza kutumika kupata muhtasari. Ili kujua mahitaji ya mtu, mtu anapaswa kukabiliana na hisia za mtu. Kwa kusudi hili, orodha ya hisia pamoja na hisia zisizotimizwa pia vinaweza kupatikana katika kiambatanisho. Kila hatua anayochukua mtu hufanyika ili kukidhi haja. Watu wote wana mahitaji sawa. Kutimizwa kwa haja hakutegemeani na watu na vitendo. Kuwasiliana na mahitaji ya mtu yasiyotimizwa humsaidia mtu kumwelewa mwenzake vizuri zaidi. Ni muhimu hapa kutenganisha mahitaji ya mtu na mikakati safi ambayo mtu anataka tu kutimiza mahitaji yake mwenyewe. Mikakati ya kujitegemea inatuingiza katika mgogoro na wengine. Kwa hiyo, hisia na mahitaji ya mtu mwingine lazima yazingatiwe kila wakati.

Hapa kuna muhtasari mfupi wa mahitaji ya msingi ya binadamu::




**Hatua ya 4: Hatua / Ombi / Matakwa**

Hatua ya nne inajumuisha kuunda ombi ambalo linaelezea njia ambayo mahitaji yangu yanaweza kutimizwa. Hapa ni muhimu kwamba mahitaji ya mpatanishi wangu pia yanaheshimiwa na kujumuishwa. Sharti la mawasiliano zaidi kufanikiwa ni kukubali na kukaribisha "hapana" kama jibu. Aidha, lazima kuwa makini kwamba uundaji wa ombi la mtu hauwezi kuchukuliwa kama madai au tishio na mtu mwingine. Ombi linaonyesha mkakati wa jinsi ningependelea hitaji langu litimizwe. Haimaanishi kwamba hii ndiyo njia pekee na sahihi ya kutimiza hitaji hili. Kwa kuongezea, pia haimaanishi kwamba ombi hili linapaswa kutimizwa kwa hali yoyote. Mtu anapaswa kukubali mahitaji ya mtu mwingine, kwa sababu kwa njia hii mtu ana uwezekano mkubwa wa kupata kile anachotaka. Katika hali yoyote haipaswi "hapana" kumaanisha matokeo mabaya kwa mtu mwingine..

→ **Hisia ni viashiria vya kama mahitaji yanatimizwa au la..**



https://pixabay.com

Kwa msaada wa vipengele hivi vinne, kila mtu anapaswa kusikiliza kwa uelewa. Mawasiliano yasiyo ya vurugu yanaweza kutumika kwa hali yoyote katika eneo lolote la maisha. Haijalishi kama ni mawasiliano ndani ya familia, shuleni, katika mahusiano ya karibu au hata katika mazungumzo ya biashara. Yanaweza kutumika katika migogoro na mifarakano ya aina yoyote. Yanatusaidia kukuza uelewa wetu katika kila hali na kuwa na ufahamu zaidi wa jinsi tunavyojieleza. Hili linaweza kuongeza ubora wa maisha yetu kwa kujenga hamu ya pamoja ya kutoa kutoka moyoni.

**Marshall B. Rosenberg anatofautisha kati ya ngazi tatu za mawasiliano:**

Hatua nne za mawasiliano yasiyo ya vurugu kulingana na Marshall B. Rosenberg zinaweza kuonekana kama mchakato ambapo uchunguzi wa hali hujenga hisia kwa sababu ya haja isiyotimizwa na hii inapaswa kutatuliwa kwa ombi. Sababu na kichocheo lazima zitenganishwe.




**Kijielewa:**

Tukifanikiwa kufahamu hisia na mahitaji yetu pamoja na hisia na mahitaji ya binadamu wenzetu, tunaweza kuona mahusiano katika mwanga mpya. Athari za kujibu migogoro kwa vurugu zinaweza kupunguzwa hadi kiwango cha chini. Kwa kuwa tuweka maanani huruma zaidi, naama umakini wetu ni juu ya huruma, kuchunguza na kuhukumu hupuuzwa

**Kusikiliza kwa uelewa**

Usikilizaji mkubwa, wenye uelewa ni muhimu kwa mawasiliano yenye mafanikio. Hii inamaanisha kuelewa kwa heshima na kuweza kufahamu uzoefu na maoni ya watu wengine. Kwa kufanya hivyo, mtu husikia kile ambacho mtu mwingine anakiona, anahisi, anahitaji na kuomba. Kusikiliza kwa kuvaa viatu vya mwenzako kunawezesha uhusiano wa kina na kuendeleza uhusiano na kila mmoja. (Rosenberg, 2011)

➔ **Uaminifu ni sharti la msingi..**



https://pixabay.com

**Usimamizi wa migogoro unawezaje kutumika kuleta mawasiliano yasiyo ya vurugu?**

Usimamizi wa migogoro unaweza kutumika kuondosha migogoro iliyopo, wakati mfano wa GfK unaweza kutumika kuzuia kikamilifu hali za migogoro. Usimamizi wa migogoro huingilia kati wakati pande mbili zina maoni tofauti yisiyopatanishika. Kwa usimamizi mzuri wa migogoro, masharti matatu ni muhimu kwa pande zote zinazohusika: Uwezo wa kukabiliana na migogoro, mawasiliano na utayari wa maelewano.
(Jiranek &edmüller, 2021)

| |
|---|
| **Udhibiti wa migogoro**<br>**Ufafanuzi:**<br>Udhibiti wa migogoro ni uwezo wa kuingilia kati migogoro iliyopo na kuisuluhisha vyema na kwa tija. |

**Mfano wa barafu**

Mfano wa barafu unatokana na nadharia ya Sigmund Freud ya utu (Sigmund Freud's theory of personality). Inaonyesha kwamba katika mawasiliano baina ya watu kuna kiwango cha ukweli (factual level) na kiwango cha uhusiano (relationship level). Kilele cha barafu juu ya uso wa maji hufanya karibu 20% ya ukubwa wote. Asilimia 80 iliyobaki imefichwa chini ya maji. Unaweza kufikiria kilele cha barafu kama kiwango cha ukweli wa mawasiliano. Katika ngazi hii, habari za ukweli na ukweli huwasilishwa kupitia maneno. Kiwango cha ukweli kinashughulikia maudhui yote ya kile kinachosemwa wakati wa mawasiliano. 80% iliyobaki inawakilisha kiwango cha

uhusiano uliofichwa na mahusiano ya ufahamu uliofichika (unconscious relationship). Kiwango hiki kinajumuisha mawazo na hisia, maadili na nia. Vipengele hivi vinaweza kuonyeshwa kwa muonesho wa sura, ishara na sauti na ni ya mawasiliano yasiyo ya maneno. Hata hivyo, asili hizi za kibinafsi haziwezi kamwe kueleweka kikamilifu na mpatanishi.

Katika kiwango cha ukweli (factual level) ni ukweli na habari tu humfikia mpokeaji wa ujumbe.



https://pixabay.com

Mtindo huu unahusishwa na mfano wa Sigmund Freud of the psyche. Katika mfano huu kuna matukio matatu: The Sub-I, The I na The It. The Sub-I inawakilisha kanuni za maadili kama vile kanuni na maadili kutoka mazingira/ulimwengu wa nje na hutoa madai juu ya The 'I'. Hii mara nyingi inaweza kuundwa na mitazamo ya msingi ya wazazi na inawakilisha amri na makatazo kutoka kwa jamii na inawakilisha mfano unaotegemea sababu. The 'I' inawakilisha kitendo halisi, yaani inategemea kanuni ya ukweli, na inapatanisha busara (rational) za the sub-I na tamaa/matamaniao ya the 'It'. The 'it' hutenda kwa misingi ya mawazo ya kawaida ya ulimwengu wa nje na huundwa na maumbile (genetics) na jamii yake. Lengo la the 'I' ni kuunda mfano wa usawa na udhibiti juu ya matukio mengine mawili. The 'I' inatuma majibu kwa ulimwengu wa nje na matendo yake. The 'It' inaakisi tamaa, mahitaji na misukumo ya mtu. Hii inatawaliwa

na hufanya madai ya kibinafsi kulingana na kanuni ya raha na hutenda kwa misingi ya vichocheo kutoka ulimwengu wa nje. Hii inaundwa na mitazamo ya kimsingi ya maumbile (genetics).

Katika mwingiliano kati ya watu, kutoelewana kunaweza kujitokeza haraka na migogoro inaweza kutokea. Haya yanaweza kutokea ama kwa kiwango cha ukweli (factual level) au kiwango cha uhusiano (relationship level). Migogoro juu ya kiwango cha ukweli hutatuliwa haraka kwa njia ya kusikiliza, maoni au maswali makini. Vichocheo vya migogoro katika ngazi ya ukweli vinaweza kuwa kwamba upande mmoja wa mgogoro haujui mada kuliko wengine au taarifa huchukuliwa kwa njia isiyo sahihi. Migogoro katika kiwango cha uhusiano ni vigumu zaidi kutatua. Hapa, suluhisho la mgogoro linahitaji kuzingatiwa na upande mwingine kwa njia ya huruma na uelewa. Kwa mawasiliano yenye mafanikio, ni muhimu kwamba migogoro itatuliwe kwa misingi ya kiwango cha uhusiano, kwa sababu hii pia inaathiri vibaya mawasiliano kwa kiwango cha ukweli. Kwa hivyo ikiwa kiwango cha uhusiano kitapuuzwa, asilimia 80 ya ujumbe halisi utaeleweka vibaya au hata kutoeleweka kabisa. (Abels & König, 2010)

**Dhana ya Harvard**

Dhana ya Harvard, iliyoanzishwa na Roger Fisher pamoja na William Ury, ina **kanuni nne za msingi** ambazo zinaweza kutumika kutatua migogoro kwa amani na kufikia matokeo ya ushindi kwa pande zote.

**1. Tenganisha watu na tatizo**

Watu na matatizo hutendewa tofauti na majadiliano ni ya ukweli tu.

**2. Tambua maslahi**

Ni muhimu kutozingatia misimamo ya juujuu bali maslahi na mahitaji ya kina.

**3. Dadavua kupata uwanda wa kuchagua (options)**

Njia zinapaswa kupatikana ili kunufaisha pande zote..



https://pixabay.co

**4. Kuweka vigezo vya haki**

Hatimaye, pande zote zinapaswa kukubaliana juu ya suluhisho moja kati ya masuluhisho yote yaliyopendekezwa, ambayo wote wanapaswa kukubali. Hatua hii inapaswa kufanywa kwa misingi ya vigezo visivyo na upendeleo ili kufanya uamuzi usioegemea upande wowote. (Schäfer, 2017)

**Njia ya 13: Udhibiti wa Migogoro:**

**Mfano wa Utatuzi wa Migogoro**

Mtindo huu wa utatuzi wa migogoro una mlolongo wa hatua sita zitakazofuatwa na pande zote zinazohusika. Mtindo huu unatokana na dhana mbili za msingi



**11. Kupunguza kasi ya utatuzi wa migogoro kwa kujumuisha wadau wote.**

**2. Utaratibu wa kushirikisha wadau kuanzia wasiwasi, ufafanuzi, kukubalika kwa wasiwasi mpaka kutafuta ufumbuzi. Njia hii inahitaji msimamizi anayewaongoza washiriki wote kupitia mchakato wa usimamizi wa migogoro, akichukua nafasi isiyoegemea upande wowote.**.

**Hatua ya 1: Fafanua maoni**

Hapa maswali yafuatayo yanahitaji kufafanuliwa: Suala ni nini? Nini kimetokea? Pande zinazohusika zilijisikiaje kuhusu hali hiyo? Makabiliano ya kwanza yalifanyika lini? Kwa nini hali ilijitokeza? Katika hatua hii ni muhimu kwamba umuhimu wa masumbufu ya upande mmoja yafikishwe upande wa pili

**Hatua ya 2: Funua kusudi lililobeba maoni**

Hatua ya pili ni kuhusu maslahi, matakwa, hofu na matumaini ya wote waliohusika. Hapa inabainika jinsi pande zote za mgogoro wanavyojisikia kuhusu mgogoro huo na ni nini cha muhimu kwao kufafanua..

**Hatua ya 3: Tambua wasiwasi wao mkuu.**

Hatua inayofuata ni kufanyia kazi yale ambayo ni muhimu sana katika mgogoro huo. Katika hatua hii, uelewa wa mtazamo na msimamo wa wengine unapaswa kuundwa. Lengo la hatua hii ni kuondokana kudhania na nadharia na kuzingatia mambo muhimu. Ni muhimu kufupisha hoja zote zilizotajwa ili kuepuka kutoelewana.

**Hatua ya 4: Fafanua umuhimu wa mambo yanayoleta wasiwasi..**

Kisha, kero kuu hupitiwa tena na kuangaliwa kwa umuhimu wake kwa pande zote zinazoshiriki. Ni vyema pande zote zikawa na uelewa wa maamuzi yaliyochukuliwa.

**Hatua ya 5: Andaa ufumbuzi wa msingi wa suala..**

Baada ya kero kuu kupitiwa na kukubaliwa na pande zote, hatua inayofuata ni kuandaa na kukusanya ufumbuzi unaowezekana. Hatua hii inaweza tu kusababisha matokeo yenye maana ikiwa nafasi za Hatua ya 3 na Hatua ya 4 ziko wazi kwa washiriki wote. Hapa mawazo yote ya utatuzi wa migogoro yanaweza kukusanywa.



**Hatua ya 6: Kuchagua suluhisho bora.**

Katika hatua ya mwisho, suluhisho bora linaamuliwa na utekelezaji wa mkakati huu wa suluhisho unakubaliwa

→ **Kanuni za udhibiti:**

Kama msimamizi, ni muhimu kuwa na mtazamo usioegemea upande wowote juu ya maudhui.

Msimamizi anapaswa kuweka wazi mgogoro ili vipengele tofauti viweze kutofautishwa na kila mmoja na kuwa wazi kwa wote.

Endelea na hatua inayofuata pale tu pande zote zinapokubaliana na hitimisho la hatua na kuridhika na matokeo.

(Jinarek & Edmüller,2021

**Maneno ya kufunga**

Kitabu hiki cha kiongozi wa vijana kimsingi kinachukuliwa kama mwelekeo wa kazi ya elimu ya uraia kwa na miongoni mwa vijana. Ni muhimu kuwa makini kutochukua pande wakati wa matumizi yake. Hii ni kwa sababu kazi ya elimu ya uraia (hasa katika Afrika ya Francophone) mara nyingi huonekana kama "kuingiza siasa" kwa vijana dhidi ya mila zilizowekwa. Kwa sababu hii, ni muhimu pia kudumisha uelewa wa watendaji wa serikali kwamba watoa maamuzi wa baadaye wanapaswa kufundishwa maadili ambayo yanahakikisha kuishi pamoja kwa amani.

Kitabu hiki si kazi iliyokamilika. Badala yake, ni rasimu ya kwanza ambayo inaweza kuchambuliwa kwa kina na kuboreshwa na watendaji wa elimu, ili kazi ya elimu ya kiraia iweze kupata nafasi miongoni mwa vijana ili kujenga jamii ulimwenguni kote ambazo zina jambo moja tu akilini: kujenga uishiji wa pamoja ulimwenguni kote kwa njia ya kudumu.

Kiambatanisho

**Vifaa vya kazi kutoka Moduli ya 1**

Awamu nne za kuunganisha [45]**:** Kuainisha kila moja ya mifano minne (upande wa kulia) kwa awamu ya kuunganisha (upande wa kushoto) kwa kuunganisha visanduku vya maandishi.

**1. Awamu ya awali ya kuunganisha**
< Majuma 6
Hadi sasa, hakuna ukaribu uliojengeka. Kwa hiyo, haimpi shida mtoto kuwa na watu wazima wasiojulikana. Mtoto huwasiliana na ishara zake za kuzaliwa (k.m. kulia, kutabasamu, kutazamana kwa macho) ili mahitaji yake yatimizwe.

James ana njaa na anapata mtindi wa kula kutoka kwa mama yake Terese. Anasikia tumbo la mama yake likiunguruma na kumuuliza "Mama, una njaa pia?" na kumpa kijiko cha mtindi wake. Mama anacheka na kusema, "Hapana, asante, nitakula supu baada ya dakika moja.

Mamake Jua ametembelewa na binamu yake Sada kwa mara ya kwanza tangu kuzaliwa kwake. Jua alizaliwa wiki chache zilizopita. Mama Jua anamuomba binamu yake amshike mtoto na kutoka chumbani kwa muda kuandaa chai. Wakati mama huyo hayupo, Jua anatazama uso wa Sada kwa shauku na kutabasamu huku akiongeleshwa naye kwa upole.

**2. Mwanzo wa kujenga ukaribu**
Juma la 6 mpaka miezi 8
Sasa, mtoto anaweza kutofautisha watu - kwa mfano, kati ya wanafamilia na watu wengine. Sasa inaonyesha tabia ya kushikamana zaidi na inaweza kupendelea mtu mmoja (k.m. mama/baba) kuliko watu wengine.

Mtoto Elias yuko nyumbani na mama yake. Mama anaenda nyuma ya nyumba ili kuanika nguo. Hivi karibuni Elias amejifunza kutembea na kumfuata mama yake nje. Huko anakaa sakafuni na kumshika mama yake. Anatabasamu, anazungumza naye kisha anaendelea na shughuli zake. Baada ya muda, Elias anainuka kucheza na mpira ukiwa chini karibu. Wakati fulani anatazama juu na kumtazama mama yake machoni.

[45] cf. (Lengning & Lüpschen, 2019, p. 14 f.)

**1. Ukaribu wa kuaminika**

Watoto waliopata ukaribu wa kuaminika wanawaona walezi wao kua wanajali, wapo karibu, wa kuaminika na kutegemewa. Kwa hiyo wanajisikia salama zaidi kuwa karibu nao, na wanaweza kuchunguza kwa uhuru mazingira yao ili mradi mazingira hayakarahishi. Kwa kuwa wametendewa kwa uzuri hata katika hali mbaya za kihisia, wanaweza kuonyesha hisia zao zote (kwa mfano, hasira, hofu) kwa uwazi.openly.

Mtoto Amaniel anakimbia kwa furaha kwenye gorofa, akiburuta toy nyuma yake, wakati mama yake anatayarisha chakula cha jioni karibu na nyumba yake. Ghafla anajikwaa, anaanguka chini na kuanza kulia. Akilia, anamkimbilia mama yake, ambaye mara moja anamkumbatia, anazungumza naye kwa faraja na kuangalia ikiwa amejiumiza. Mara Amaniel ametulia na anataka kuendelea kucheza.

**2. Ukaribu wa kutokujiamini na kuepukwaepukwa**

Watoto walio kwanye ukaribu wa kutokujiamini na kuepukwaepukwa wanawaona watu walio karibu nao kama wanaowakataa na kuwajali. Ili kuepuka kukataliwa tena, wanakwepa mahusiano na hawataki ukaribu na walezi wao hata katika hali mbaya. Badala yake, wanachunguza mazingira yao (k.m. vinyago). Kwa kuwa wamejifunza kutoungwa mkono wakati wana hisia hasi, wana ufikiaji mdogo wa hisia zao na hawaonyeshi tena wakati wanahisi hasira, hofu au huzuni, kwa mfano kuhisi hasira, hofu au huzuni,

Small Talisa yuko kwenye chumba cha kusubiri na mama yake. Talisa ameketi pale sakafuni na anaendelea kugonga mguu wa kiti na toy. Mara mama yake anainuka huku akiwa amekasirika na kutishia "Ukiendelea hivi nitakuacha hapa!" na kuondoka chumbani kwa dakika chache ili kupiga simu. Talisa anaanza kutikisa sehemu ya juu ya mwili wake na kurudi tena na tena. Mama anaporudi, Talisa kwanza anamsogelea kidogo kisha anakaa chini. wieder auf den Boden.

Mifano minne ya kuunganisha [46]**:** Kuainisha kila moja ya mifano minne (upande wa kulia) kuwa mfano wa kuunganisha (upande wa kushoto).

**3. Ukaribu usioaminika wala kueleweka**
Watoto walio na uhusiano usio salama wanaona walezi wao kama wasiotabirika kwa kuzingatia kujali na kupatikana kwao. Kwa hivyo walezi hujibu mahitaji ya mtoto bila kutabirika - k.m. wakati mwingine kwa kujjali na wakati mwingine tofauti. Watoto hawa mara nyingi hupenda sana kwa muda mrefu na hawana nia ya kuchunguza mazingira yao. Hata hivyo, wao si tu kutafuta ukaribu na mlezi wao, lakini pia wanaonyesha (kwa uwazi sana) hasira yao kwa mtu kutokana na kushindwa kukidhi mahitaji yao.

**4. Ukaribu usioeleweka (disorganized bonding)**
Watoto walio kweny ukaribu usio na mpangilio (Disorganized bonding) wamejionyesha kuwa hawana msaada katika hali zinazoleta wasiwasi na walezi wao ni kama watu wasiotoa usalama katika hali hizi. Kwa kawaida wengi wa watoto hao ni walitelekezwa na walezi wao, wakitishiwa kutengana au kunyanyaswa. Kwa hiyo walezi wenyewe wanaweza kuwa chanzo cha wasiwasi. Katika hali ngumu kihisia (k.m. kujitengwa na mtu uliye na ukaribu nae), mara nyingi huonyesha tabia za ajabu na vurugu (k.m. kufanya harakati sawa kila wakati).

Baba ya John anatembelewa na rafiki yake Zahir mara moja kwa mwezi. John ana umri wa miezi michache na amecheza na Zahir mara nyingi alipokuja kutembelea. Leo, John ghafla anaanza kulia wakati akicheza. Zahir anajaribu kumfariji, lakini mvulana mdogo hajiruhusu kutulizwa. Baba yake anapomkumbatia hatimaye, John anaacha kulia na kutulia haraka.

Yilma mdogo anataka kupakatwa mikononi mwa babake. Wakati mwingine babake anapenda kumpa ukaribu anaohitaji, lakini mara nyingi yeye hukasirishwa na kung’ang’niwa nae na hujibu kwa kutojali. Yilma anapoonyesha mahitaji yake, huwa hajui jinsi baba yake atakavyoitikia. Anang'ang'ania mguu wa baba yake na anasema kwa hasira "Achia mguu, cheza peke yako sasa." Lakini Yilma hana hamu ya kucheza peke yake na anaanza kulia na kupiga mayowe kwa sauti kubwa huku baba yake akimgeukia. Anamfuata huku akilia na baada ya muda anamkumbatia. Hata hivyo, inamchukua muda mrefu kutulia.

David mdogo ameketi sakafuni nyumbani, akicheza peke yake na toy zake. Baba yake ameketi dirishani akisoma gazeti. Ghafla, David anapata ananasa kidole chake wakati akicheza na inamuumiza sana. Kwa kua David anajua kuwa baba yake uwa anagomba kwa hasira kila Daudi anapoanza kulia. Kwa hivyo, haonyeshi hisia zake, anapuuza maumivu yake na anaendelea kujishughulisha na vitu vyake vya kuchezea.

[46](Julius, Gasteiger-Klicpera, & Kißgen, 2009, p. 14 f.)

## Muhtasari: Hisia za msingi [47]

| Kuhisi | Msingi (Fundamental) | Ufahamu (awareness) | Mwitikio wa mwili (Body reaction) | Unahitaji hatua |
|---|---|---|---|---|
| **Furaha** | Inatuwezesha kufurahia hapa na sasa, ina kitu chepesi na mara nyingi huambukiza. | Unapojawa na furaha, unaona mambo kwa undani zaidi na unashangazwa na vitu vidogo vidogo ambavyo kwa kawaida ungevipuuza | Unajisikia kuchangamka kidogo, mchapakazi na wakati mwingine "mpana". Unacheka na wakati mwingine unakuwa na mawasiliano sana au ya kuchekesha na ya utani kidogo | Hakuna matendo yaliyoelekezwa moja kwa moja - na huo ndio uzuri wa furaha. Unataka kufurahia wakati na kushiriki furaha yako na wengine. |
| **Upendo** | Upendo huhusisha hisia nyingi tofauti, kama vile mapenzi, hamu ya ngono na mshikamano mkubwa kwa watu au viumbe vya juu, kama vile Mungu. Tunazingatia hapa kwenye mapenzi | Mtazamo wetu umepungua kwa sababu tunaona hasa pande chanya za mwenzi wetu. | Miitikio ya mwili haiko maalum. Kuwa katika mapenzi kunatufanya tuhisi kujaa nguvu, wepesi na waliosisimka. | Tunataka kwa haraka kujenga ukaribu na mtu tunayempenda. Na tunataka kuwa na maana maalum kwa mtu kama alivyo kwetu.. |
| **Fahari** | Tunajisikia fahari wakati sisi - au mtu ambaye tunahisi kushikamana naye - ametenda jambo flani kwa mafanikio. | Fahari inakufanya ujisikie vizuri sana na kujithamini zaidi. Unakua huru zaidi (carefree), mwenye nguvu na uwezo. | Unajisikia mwepesi zaidi, mwenye furaha na umejaa nishati. Mwili unataka kunyooka na kushikilia kichwa chake juu.. | Unapojivunia, unataka kujionyesha na kupata shukrani kwa utendaji wako. |
| **Raha na hamu / "** | Kutamani" Raha sio tu kwa ngono. Chakula, muziki, madawa ya | Kadri lengo la tamaa yetu linavyozidi kuwa karibu, ndivyo | Tunaelekeza mawazo na nguvu zetu katika kutimiza | Msukumo wa kutenda unategemea nini kilikuwa |

[47] cf. (Bohus & Wolf, 2009, p. 200-244)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
